


**YANGA HAOOO ROBO FAINALI KLABU BINGWA**

UKURASA 24

**Aliyeachiwa** kwa msamaha wa Rais aiba tena, atupwa gerezani miaka 30

UKURASA 3

**MAISHA YALIVYO**

**Ulimwacha** mke, unataka arejee akiwa kimada

UKURASA 11

**Msako** walanguzi wa sukari wazidi kutikisa mikoani

UKURASA 2

**Wanafunzi waonywa janga unywaji pombe** UK. 5


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581597

Jumapili Februari 25, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


# Madudu viwandani

• **Chenye** leseni ya kuzalisha mabati, chabainika kinauza majokofu, vigae, PVC... *Endelea Ukurasa 2*



Waziri wa Viwanda na Biashara Dk. Ashatu Kijaji






Rais Samia Suluhu Hassan akiwa pamoja na viongozi wa nchi mbalimbali kwenye mazishi ya kitaifa ya aliyekuwa Rais wa Namibia, Hayati Dk. Hage Geingob katika uwanja wa michezo wa Uhuru, jijini Windhoek, Namibia jana. **PICHA NDOGO:** Jeneza lenye mwili wa Hayati Dk. Hage Geingob likiwasili katika uwanja huo. **PICHA: IKULU**

## Watoto wengi hatarini kuugua kiharusi nchini

UK. 4

UKURASA 3

## Haki za punda zinavyokiukwa kila kukicha



**MICHEZO** MASHINDANO KUOGELEA YASHIKA KASI DAR UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6




Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akikagua mabati yanayozalishwa na kiwanda cha Dragon, alipotembelea kiwandani hapo, jijini Dodoma juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waziri abaini madudu viwandani

**Na Joseph Mwendapole**

NI 'madudu' viwandani! Ndicho unachoweza kusema kutokana na kilichobainika katika ziara ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji jijini Dodoma juzi.

Kiwanda kilichopewa leseni na serikali kuzalisha mabati, kimebainika kinauza majokofu, vigae, PVC na bodi za dari (ceiling boards).

Kutokana na kadhia hiyo, waziri huyo ameagiza taasisi za serikali kupita kwenye viwanda vyote nchini vinavyozalisha mabati na bidhaa nyingine kukagua kama bidhaa zinazozalishwa na viwanda nchini zinakidhi viwango.

Taasisi zilizopewa maagizo hayo ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Shirika la Viwango Tansania (TBS) na Wakala wa Vipimo (WMA).

Waziri Kijaji alitoa maagizo hayo juzi jijini Dodoma alipozuru kwenye viwanda vya kuzalisha mabati vya ALAF na Herosean Enterprises inayozalisha mabati ya DRAGON ikiwa ni utekelezaji maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Rais Samia alishaagiza kuwa viongozi wanapaswa kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa na viwanda nchini, zinazingatia ubora.

Waziri huyo akiwa kwenye kiwanda cha Herosean Enterprises, alibaini kuwapo bidhaa zingine ambazo hazihusiani na malengo halisi ya leseni iliyotolewa na BRELA.

"Leo (juzi) nimetembelea viwanda hivi viwili lakini cha kusikitisha hiki kiwanda cha kuzalisha mabati ya DRAGON kinajihusisha na biashara ya kuuza bidhaa nyingine ikiwamo friji, PVC, vigae na ceiling boards (bodi za dari).

"Nimewataka wanioneshe vielelezo vya usajili wa bidhaa hizo tofauti na bidhaa za mabati kiwandani hapa, sikupata majibu sahihi.

"Ninaziagiza taasisi zinazohusika na hili suala zilishughulikie ili kupata ukweli wake," aliagiza Waziri Kijaji aliyefuatana maofisa kadhaa toka wizara yake.

Vilevile, Waziri Kijaji aliagiza wamiliki wa viwanda vinavyozalisha bidhaa za mabati nchini, kuuza bidhaa hiyo kwa bei rafiki ili kunufaisha wanunuzi kwa makundi yote.

"Jambo lingine ninalotaka kuwaambia watanzania kwa bidhaa nilizotembelea leo, ukilinganisha na nchi zingine, mabati yetu Tanzania bei yetu iko chini kuliko nchi yoyote ile ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, hivyo niwatake msisikilize kelele za mtaani, endeleeni kujenga kwa wingi na sisi serikali tunaendelea kutekeleza miradi yetu," alisema Dk. Kijaji.

Ofisa Huduma kwa Wateja Kiwanda cha Mabati ya ALAF, Herry Jailos, alishukuru serikali kwa kufanya ziara na kubaini changamoto zinazowakabili ikiwamo ukosefu wa masoko kutokana na wazalishaji bidhaa hizo kuwa wengi nchini.

Kiwanda kubainika kuwa na bidhaa ambazo hakina leseni ya uzalishaji wake si tukio jipya nchini. Novemba 3, mwaka jana, serikali ilibaini kuwa kiwanda cha kampuni ya Toco & Company Limited kilikuwa kinazalisha mifuko ya plastiki iliyopigwa na serikali ilihali kina leseni ya kuzalisha mifuko ya plastiki yenye ubora unaotakiwa.

Vilevile, ilibaini wakati wa ukaguzi kiwandani huko, Mbezi Juu, wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, kwamba kiwanda cha kampuni hiyo iliyosajiliwa nchini Oktoba 19, 2019, kilikuwa na mabango nje ya kiwanda yanayoonesha kinazalisha mabati ilhali usajili wake ni wa kuzalisha mifuko kwa ajili ya vifungashio visivyoharibu mazingira.

Juni Mosi, 2019, serikali ilianza kutekeleza rasmi marufuku ya kuzalisha, kusambaza na kutumia mifuko ya plastiki.

# Wawekezaji wa Misri waitwa kuwekeza viwanda vya sukari

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imehimiza wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Misri kuwekeza katika viwanda vya kuzalisha sukari nchini.

Lengo ni kuzalisha bidhaa hiyo nchini badala ya kuendelea kuuziwa iliyozalishwa nje ya nchi, ilhali kuna mazingira wezeshi ya kujenga viwanda vya uzalishaji.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa kongamano la wafanyabiashara wa Misri na Tanzania.

Alisema serikali ingependa kuona wafanyabiashara hao wanazalisha bidhaa nchini kwa manufaa ya watanzania na waafrika.

"Tumeona kuna haja ya kupunguza bidhaa zinazoingia ili tuwe na bidhaa zinazotoka kwenda soka la nje na hivyo itawezekana kama tukiwa na wawekezaji hao nchini kwetu," alisema.

Kigahe alisema eneo mojawapo walilovutiwa wafanyabiashara hao ni huduma ya ndege za kubeba mizigo. Mwakilishi kutoka Shirikisho la Viwanda Misri (FEI) Dk. Sharif Elgabaly, alisema moja ya maeneo yaliyowagusa ni kusikia Tanzania kuna kiasi kikubwa cha gesi.

Alisema gesi inaweza kuwa na maana kwa nchi kama serikali itatengeneza mipango thabiti ya kuhakikisha inatolewa baharini kuletwa nchi kavu.

"Nikilinganisha Tanzania na Misri, ninaona fursa kubwa kwa Tanzania kuendelea kwa viwanda kwa sababu ya kuwapo rasilimali ikiwamo ujazo mkubwa wa gesi ambao unatosha kuendesha na kusuma viwanda," alisisitiza Dk. Elgabaly.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Gilead Teri, alisema lengo la kukutanisha wawekezaji wa pande mbili ni kuwaonesha fursa za uwekezaji zilizomo nchini na kuwahamasisha kushirikiana ili kufanya uwekezaji wa pamoja.

"Miaka ya karibuni uwekezaji wa Misri nchini umeongezeka kutokana na ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan Misri mwaka 2021. Alivutia kampuni kutoka Misri kuja kuwekeza na sasa wapo wengine wamekuja kuangalia maeneo," alisema.

Takribani kampuni 50 kutoka Tanzania na 10 kutoka Misri zilikutana kwenye kongamano hilo kutoka sekta za dawa, bidhaa za nyumbani, ujenzi, miundombinu na kilimo.

# Msako walanguzi sukari wazidi kupamba moto

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KAMATI ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Singida imefanya operesheni ya ukaguzi wa maduka ya jumla ya wafanyabiashara wanaouza sukari mjini Singida, ikionya kuwa yeyote atakayebainika anauza sukari kwa bei kubwa kinyume cha bei elekezi atakamatwa na kufunguliwa mashtaka ya uhujumu uchumi.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, aliyeongoza kamati hiyo juzi, baada ya kufanya ukaguzi huo, aliagiza wakuu wa wilaya ndani ya siku tatu kila mmoja akafanye ukaguzi kwenye maduka ya wafanyabiashara wanaouza sukari katika wilaya zao kubaini bei wanazouza bidhaa hiyo.

Ukaguzi huo umefanyika ikiwa ni siku moja baada ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, kutoa agizo kwa wakuu wa mikoa kusimamia usambazaji sukari na kuchukua hatua dhidi ya wafanyabiashara wote wanaohujumu upatikanaji wake.

"Niwaombe wakuu wa wilaya, kila mtu aende kwenye wilaya yake na halmashauri yake kwenye maduka yanayouza sukari kufanya ukaguzi kuomba bei za ununuzi ili kujua kama ameuzia bei ya kawaida au la kutoka kwenye maduka ya jumla na waoneshe risiti atakayesema hana risiti huyo tumpeleke moja kwa moja tukamfungulie mashtaka ya uhujumu uchumi," aliagiza.

Serukamba pia aliagiza wafanyabiashara wote walionunua sukari kutoka kwa msambazaji mkuu wa Mkoa wa Singida watakaosema sukari imekwisha waoneshe risiti jinsi walivyoiuza na watakaoshindwa kuonesha risiti waingizwe kwenye kosa la kufanya biashara bila kutoa risiti.

"Mfanyabiashara atakayeshindwa kutoa risiti maana yake huyo atakuwa anayo lakini atakuwa ameamua kuificha ili auze bei kubwa, huyo naye tumfungulie mashtaka ya uhujumu uchumi na wale watakaotoa ushirikiano kutoa risiti tuangalie kwa wale waliowauzia ili tushughulike nao," alisema.

Serukamba pia aliagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Singida kutoa nakala za risiti zote za wafanyabiashara wa maduka ya jumla walivyouza sukari ili kuangalia kama zinawiana na zile ambazo walipewa wafanyabiashara wa maduka ya kati na rejareja hao kama itakuwa tofauti, hatua zichukuliwe.

"Sukari itaanza kuingia, Ofisa Biashara wa Mkoa hakikisha unasimamia msambazaji mkuu wa sukari jinsi anavyogawa sukari maana hapa tumeona anawauzia wafanyabiashara wenzake wa mjini ili nao wakalangue watu wengine wakati inatakiwa kila wilaya ipate mgawo sawa," alisema.

Mmoja wa wafanyabiashara wa maduka ya jumla, Muhsin Damji, alishauri serikali badala ya sukari kuagizwa na wafanyabishara wachache wanaopewa vibali na serikali, itoe rukhsa kila mfanyabiashara mwenye uwezo aagize sukari hata kutoka nje , mradi tu alipe kodi ya serikali kama inavyotakiwa.

Baada ya kamati hiyo ya ulinzi na usalama kufanya ukaguzi katika maduka ya jumla ilibaini bei za sukari kwa wafanyabiashara hao ni kati ya Sh. 140,000 na 145,000 kwa mfuko wenye ujazo wa kilo 50.

Meneja wa TRA Mkoa wa Singida, Azaria Kasomi, alisema ukaguzi wa risiti kwenye maduka utaendelea kufanyika na atakayebainika hajatoa, atatozwa faini ya Sh. 1,500,000.

HABARI KITAIFA

# Haki za punda zinavyokiukwa nchini

**Na Thobias Mwanakatwe,** DODOMA

SHIRIKA lisilokuwa la kiserikali la Inades Formation Tanzania (IFTz) linalojishughulisha na maendeleo ya kijamii, kiuchumi na ustawi wa kijamii limeomba serikali kuingiza mnyama punda katika mtaala wa masomo ya ustawi wa wanyama.

Limesema hatua hiyo itasaidia wataalamu wanaohitimu vyuo vya afya na tiba ya mifugo kuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa mnyama huyo.

Daktari wa Afya na Tiba ya Wanyama wa shirika hilo, Dk. Charles Bukula, akizungumza wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari juzi mjini hapa, alisema mtaala wa Tanzania haujamzungumzia punda kama ilivyo kwa wanyama wengine kama farasi.

Alisema hali hiyo ni dosari kwa ustawi wa punda kwa kuwa inasababisha mnyama huyo akose haki za msingi ikiwamo matibabu.

Alisema kukosekana wataalamu wa mnyama punda kunasababisha changamoto nyingi, ikiwamo kutokaguliwa nyama ya punda anapochinjwa. Hivyo, ikitokea mtumiaji amepata madhara hawezi kupata msaada wowote.

Alisema kuwa serikali pamoja na wadau wa ustawi wa wanyama wanapaswa kupitia upya kanuni za ustawi wa wanyama ili punda kujumuishwa kama mnyama anyayeonekana kuwa haarini kutoweka.

"Ifike wakati jamii imthamini punda kama inavyothamini wanyama wengine kwa kumpatia matibabu, lishe bora na kutosababishiwa maumivu yasiyo ya lazima, mfano kupigwa ovyo wakiamini kuwa punda haumii," alisema.

Dk. Bukula alisema katika kuendelea kumthamini punda, serikali itenge mwezi Mei kuadhimisha siku ya punda duniani ambayo itakuwa inaadhimishwa kila mwaka kama wanavyoadhimisha siku ya ugonjwa wa kichaa duniani kwa lengo kutoa hamasa kubwa kwa punda kupewa thamani kama wanyama wengine.

Aliongeza kuwa shirika la IFTz linatambua kuwa kama punda akistawi, jamii itamtumia kwa muda muda mrefu na kupata kipato pale anapotumika katika shughuli za usafirshaji mizigo.

Alisema punda kama ilivyo kwa wanyama wengine, anazo haki ambazo ni pamoja na haki ya kutopata njaa, kiu au udhoofu wa mwili, haki ya kupewa chakula bora na maji ya kunywa, haki ya kuwa huru dhidi ya hofu na msongo wa mawazo na haki ya kutosumbuliwa kifikra.

Nyingine ni haki ya kuwa huru dhidi ya usumbufu wa mwili wake, haki ya kuwa huru dhidi ya maumivu, majeraha na magonjwa na pia ana haki ya kukingwa dhidi ya maradhi, majeraha au maumivu.

Shirika la IFTz linaendesha mradi wa kuboresha maisha ya jamii kupitia ustawi wa mnyama punda kwa ufadhili wa Shirika la Brooke East Africa, mradi ambao unaendeshwa katika mikoa ya Dodoma, Iringa na Singida. Malengo mahususi ya mradi huo ni kubadilisha na kuboresha ustawi wa punda wanaofanya kazi katika jamii, kuwasaidia katika kustawi na kuendeleza ustahimilivu zaidi, kuongeza vishawishi ili kusaidia kuingizwa kwa mahitaji ya punda katka sera na desturi ikiwa ni pamoja na maandalizi ya maafa na dharura.

Malengo mengine ni kutengeneza mifumo thabiti ya afya ya wanyama inayokidhi mahitaji ya haraka na ya baadaye kwa punda wanaofanya kazi.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki (kulia), akikabidhi tuzo maalum kwa Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Kasilda Mgeni kama ishara ya kutambua mchango wake katika kuhamasisha Utalii, wakati wa uzinduzi wa Tamasha la Same Utalii jana. Katikati ni Mkuu wa wilaya ya Mwanga, Abdallah Mwaipaya. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

## Aliyeachiwa kwa msamaha wa Rais ahukumiwa miaka 30 jela

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

JOHN Chibuga (31), mkazi wa Kijiji cha Bugolola wilayani Ukerewe, mkoani Mwanza, ambaye Desemba 9, mwaka jana aliachiliwa kwa msamaha wa Rais, amehukumiwa kifungo cha miaka 30 gerezani baada ya kukutwa na kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Aidan Nziku, alidai kuwa Chibuga alimvamia Mdala Mangu (34), mkazi wa Ukerewe akiwa nyumbani kwake na kumkata kwa panga sehemu mbalimbali za mwili wake kisha kuiba simu ya mkononi na kukimbia.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Ukerewe, Lucas Nyahega, aliyesema kuwa ushahidi uliotolewa mahakamani huko haukutia shaka, mshtakiwa alitenda kosa hilo kwa kukusudia na hivyo mahakama inamhukumu kwenda gerezani kutumikia kifungo cha miaka 30.

Awali Mwendesha Mashtaka wa Serikali Nziku akisoma mashtaka hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa mahakama hiyo, alidai mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Desemba 15, 2023 katika Kijiji cha Kakerege, wilayani Ukerewe.

Alidai kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa la namna hiyo kwa mara ya pili ambapo awali alihukumiwa kwa kosa la kuvunja duka usiku na kuiba, hivyo kutiwa hatiani na Mahakama ya Mwanzo Nansio kisha kuachiliwa huru Desemba 9, 2023 kwa msamaha wa Rais.

Alidai kosa hilo la unyang'anyi wa kutumia silaha ni kinyume cha kifungu namba 287(A) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura 16 (2022), hivyo kuiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali dhidi yake ili iwe fundisho kwa watu wengine.

Mshtakiwa huyo alipopewa nafasi ya kujitetea kutokana na kosa linalomkabili, aliomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa hakuwa na fedha ya kujikimu baada ya kutoka gerezani, ndiyo sababu ya kupora.


**IN THE DISTRICT DELEGETE COURT OF KOROGWE AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 8828 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE BEATRICE DAUDI KALUGENDO**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY PEACE DAUD KALUGENDO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 25th day of March 2024.
No will of the said deceased is deposited at this court.
DATED at KOROGWE this 23rd day of February, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO**

**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...4/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: JUMA JOHN HENRY wa KIHONDA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SHAMTE JUMA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 02 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 25 mwezi 01 mwaka 2024

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
**40470DODOMA,**

........Tarehe 23 FEB'2024

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 24 FEB' 2024 kampuni ya TRANSCARGO LTD itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA, gari hilo lenye namba za usajili: T397CYN/T671EAE/T676EAE
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 22.50 |
| Upana | - | mita | 4.20 |
| Kimo | - | mita | 4.60 |

3. Njia itakayotumika: DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA Kupitia MOROGORO

gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NAMBA 26010 YA MWAKA 2023**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU FELIX FRANCIS KESSY**
**AGNES FELIX KESSY..............................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 04 mwezi wa 03, 2024.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 20 mwezi wa 02, 2024.

NAIBU MSAJILI

**Summons to appear (O.VR.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**Misc. Land Application No. 2242 of 2024**

**IKU BROWN KASESE......................APPLICANT**

**VERSUS**

**JEAN LUC SABATO ...............RESPONDENT**

**TO: JEAN LUC SABATO**

**WHEREAS:** The above named **APPLICANT** has instituted an **APPLICATION** against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent on 28th day of February, 2024 at 10:00am for hearing Before **Hon. M. GWAE JUDGE** to answer the said **APPLICATION** and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your reply.
**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day the said matter will be heard and determined in your absence.
**GIVEN UNDER MY HAND** and the seal of this Court, this 20th day of February, 2024.

DEPUTY REGISTRAR

# Kamati ya Bunge yaridhishwa huduma Muhimbili-Mloganzila

**Na Christina Mwakangale**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi imeridhishwa na huduma zinazotolewa na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Faustine Ndugulile alieleza kuridhishwa na utendaji wa hospitali hiyo jana mkoani Dar es Salaam baada ya wajumbe wa kamati kuzuru hospitalini huko.

Alisema vifaa vya kisasa ikiwamo mazingira safi na rafiki yanayoelezewa na wagonjwa waliozungumza na wajumbe wa kamati hiyo, vinadhihirisha huduma zitolewazo ni rafiki, hivyo jamii isitilie shaka huduma za hospitali hiyo.

"Kumekuwa na dhana potofu mitaani kwamba mgonjwa anayeingia Mloganzila uwezekano wa kutoka salama ni mdogo. Tumefanya ziara Mloganzila, kama Kamati ya Bunge tumeridhishwa, tuwadhihirishie wananchi kuiamini hospitali hii," alisema Dk. Ndugulile.

Alisema eneo hilo linahitaji kuongezwa uwekezaji ingawa changamoto ni kutorasimishwa rasmi ardhi ya eneo hilo yenye takribani ekari 3,000 iliyo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

"Tunahitaji kuongeza wigo wa utoaji huduma, eneo hili ni kubwa, kamati tunataka Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya kukaa chini na kukubaliana kuhusu eneo hili, ili ujenzi wa majengo mengine uendelee," aliagiza Dk. Ndugulile.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema uwekezaji katika afya umeongeza mapato, ikiwamo katika hospitali hiyo ambayo hadi sasa kwenye tiba urembo imeingizia MNH Sh. bilioni nane kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu tangu huduma ianzishwe.

"Kuna upasuaji unafanyika wa kibingwa nchini badala ya watu kufuata nje. Fedha MNH wanazopata wanaweza kufanya maboresho katika maeneo tofauti ya kutolea huduma," alisema Dk. Mollel.




Mwendesha guta akiwa amelisheheni kwa mzigo wa vipande vya magodoro katika eneo la ITV Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana na kumfanya ashindwe kuona nyuma kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Wataalamu: Watoto wengi watakumbwa baa la kiharusi

**Na Mary Geofrey**

WATAALAMU wa tiba nchini wametoa angalizo la watoto wengi kuugua kiharusi miaka 10 ijayo kutokana na kutoshughulisha miili kwenye michezo.

Ugonjwa huo umekuwa ukikumba watu wazima kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo mtindo wa maisha, magonjwa yasiyoambukiza kama vile kisukari na shinikizo la damu na msongo wa mawazo.

Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Dk. Omari Ubuguyu, ndiye ametoa angalizo la hatari ijayo.

Amesema kuwa baada ya miaka 10 ijayo, magonjwa yasiyoambukiza kwa watoto wenye umri kuanzia miaka mitano hadi miaka 18 wasioushughulisha mwili kwa michezo, yataongezeka.

Kwa mujibu wa Dk. Ubuguyu, kutokana na kutoushughulisha mwili, kundi hilo liko hatarini kupata magonjwa yasiyoambukiza kama kiharusi, shinikizo la juu la damu, moyo na saratani.

Alisema takwimu za Wizara ya Afya zinaonesha kuwa, ni watoto wawili kati ya 10 sawa na asilimia 20 ya watoto wote wanaofanya mazoezi ya mwili, huku asilimia 20 wakiwa hawafanyi kabisa na hivyo kuwa katika hatari ya kupata magojwa hayo.

Dk. Ubuguyu anabainisha hayo katika mazungumzo mahususi na mwandishi wa habari hizi jijini Dar es Salaam.

Ni wakati wa kongamano la kujadili tabia hatarishi za magonjwa yasiyoambukiza na njia za kuyadhibiti.

Kongamano hilo lilishirikisha Wizara ya Afya, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Baraza la Michezo la Taifa, vyama vya michezo, walimu na wataalamu wa michezo kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

Dk. Ubuguyu alisema watoto wadogo hutakiwa kushughulisha mwili angalau kwa dakika 60 mara moja kwa siku na, au mara tano kwa wiki.

Alitaja sababu za watoto kuwa hatarini kupata magonjwa hayo kuwa ni kukaa sehemu moja kwa muda mrefu kwa shughuli za kujisomea au michezo ya kutumia simu na televisheni.

"Watoto wana hali ngumu zaidi na ndio walioko shuleni, tunawalenga sana kama kundi maalum tunalolilenga kwa ajili ya kuhamasisha kushiriki michezo inayoshughulisha miili yao na kuondokana na tabia bwete. Siku hizi si ajabu kuona mtoto ana kilo nyingi zinazolingana na za mtu mzima," alisema.

Alisema kundi hilo ni la kuangalia zaidi kwa kuwa katika kipindi cha miaka 10 ijayo, litaanza kuugua maradhi hayo.

Dk. Ubuguyu alisema kundi la pili ni la watu wote; wazee na wafanyakazi kwa kuwa hawapati nafasi ya kufanya mazoezi na wagonjwa walioko hospitalini wanaolala muda mrefu.

Kundi lingine, daktari huyo alisema ni watu wenye ulemavu, wanapaswa kufanya mazoezi ili kujikinga na magonjwa hayo.

Alisema athari za magonjwa yasiyoambukiza zinaanza kuonekana katika umri wa miaka 40 na kuendelea wakati vichocheo vyake vinaanza miaka 10 nyuma, lakini wengi wanashindwa kubaini kwa kuwa hawana utaratibu wa kupima afya mara kwa mara.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa katika kila watu 11, mmoja (asilimia 9.1) ana ugonjwa wa kisukari (utafiti wa mwaka 2012).

Mtaalamu huyo wa magonjwa aliendelea kubainisha kuwa katika kila watu wanne, mmoja anashinikizo la juu la damu na kila mwaka, watu 40,464 hunaugua saratani na kati yao, 26,000 hufariki dunia.

Alisema kuwa kupitia mkutano huo ulioshirikisha wadau wa michezo, walitarajia kuweka mikakati ya pamoja kumwezesha kila mtanzania kushiriki michezo kama kutembea, kucheza rede na mingine inayomwezesha kuepuka magonjwa hayo.

Mratibu wa Shirikisho la Magonjwa Yasiyoambukiza, Happy Nchimbi, alisema wanashirikiana na serikali kuhamasisha na kuhimiza sera zinazopambana na kujikinga na magonjwa hayo.

Happy pia alisema wanaelimisha jamii na makundi mbalimbali ya walimu, wanafunzi, wafanyakazi na kusaidia wenye magonjwa hayo kupata msaada wa kisaikolojia.

Alisema kwa watoto wenye magonjwa ya kisukari, hatua ya kwanza wamewasaidia kupata dawa na kuwapatia vitendea kazi vya kupima sukari wakiwa nyumbani.

Mnamo Agosti 2022, uongozi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ulibainisha kuwa ulitumia Sh. bilioni 99.09 kugharamia matibabu ya wanachama waliougua magonjwa yasiyoambukiza kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Kiwango hicho ni sawa na asilimia 18 ya fedha zote zilizolipwa katika kushughulikia magonjwa sugu huku dawa za saratani na huduma za kusafishwa figo 'dialysis' zikitumia fedha nyingi zaidi.

HABARI KITAIFA

# Maji ya Ziwa yameza makazi na mashamba

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

WAKAZI wa vitongoji vya Itindi na Kamchanga katika Kijiji cha Sontaukia, wilayani Sumbawanga, mkoani Rukwa wamelazimika kuyakimbia makazi yao baada ya nyumba zao kumezwa na nyingine kubomoka kutokana na maji yanayotoka Ziwa Rukwa.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Laban Sichone alimwambia mwandishi wa habari hizi jana kuwa zaidi ya kaya 500 zinazokadiriwa kuwa na wakazi 1,500 katika vitongoji hivyo zimelazimika kuhama kutokana na nyumba zao kumezwa na maji yanayoendelea kuongezeka siku hadi siku yakitokea ziwani.

Alisema kuwa kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha mkoani Rukwa na maeneo jirani maji yamekuwa yanatiririka kuelekea Bonde la Ziwa Rukwa hadi ziwani kwenyewe.

Aliitaja ni hali inayosababisha ziwa kujaa hadi kufurika na maji kufikia vijiji vilivyoko pembezoni mwa ziwa hilo. Huko ndiko nyumba na mashamba ya mpunga ya wakazi hao yamemezwa na maji.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa kutokana na maji hayo kuzingira makazi, nyumba zimekuwa zikianguka huku watu wakishindwa kuishi kwenye mafuriko na kulazimika kuhama na mali zao ikiwamo mifugo na kuomba hifadhi maeneo ya mbali.

"Hali hii inatokana na uharibifu wa mazingira uliosababisha mchanga kujaa ziwani na kina cha ziwa kimekuwa kifupi, ndiyo maana imekuwa rahisi kwa ziwa kufurika maji na sasa imeleta athari kubwa kwa wananchi licha ya kuwa miaka mingi tumekuwa tukiwashauri kuhama maeneo hayo lakini walikuwa wanakaidi," alisema.

Mmoja wa wakazi waliohama kutoka Kitongoji cha Kamchanga, Devotha Shija alisema wamelazimika kuhama kwa kuwa maji yamewafuata na kuhatarisha maisha yao; nyumba zinaanguka na kuna hofu ya kuibuka magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu.

Diwani wa Mtowisa, Edger Malini alisema ametoa taarifa kwa Kamati ya Maafa ngazi ya wilaya ili ione ni kutoa msaada kwa wananchi hao ambao hivi sasa wanapitia kipindi kigumu hasa wanawake na watoto kwa kuwa mvua inaendelea kunyesha.

# Wanafunzi waonywa janga unywaji pombe

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KUNA kilio cha kuwapo idadi kubwa ya wanywaji wa pombe nchini, Tanzania ikitajwa kuwa miongoni mwa nchi tatu zenye wanywaji wengi zaidi barani Afrika.

Kuwa na hali hiyo inayonyooshewa kidole, onyo limetolewa kwa wanafunzi wa shule za sekondari kujiepusha na unywaji pombe chini ya umri ili kulinda afya zao na kujihakikishia kufanya vizuri kwenye masomo yao.

Kampeni hiyo muhimu iitwayo SMASHED iliyoanzishwa katika Shule ya Sekondari ya Msasani katika mapambano dhidi ya unywaji pombe chini ya umri, iko chini ya kampuni ya Serengeti Breweries Limited (SBL).

Kampeni hiyo ilizinduliwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kisare Magori, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ambaye alisisitiza azma ya pamoja ya kulinda ustawi na mustakabali wa kizazi cha vijana wa kitanzania.

"Ni faraja kuona kampuni ya bia ikipigania dhidi ya unywaji pombe chini ya umri, SBL wanatoa mfano mzuri sana kwa jamii. Ninatumaini kwamba tunaweza kujifunza na kushirikiana nao ili kulinda vizazi vyetu vijavyo dhidi ya unywaji pombe chini ya umri," alisema.

Aliongeza kuwa programu hiyo inatumia tasnia ya uigizaji kuangazia suala linalojitokeza katika jamii la matumizi ya pombe chini ya umri na athari zake hasi kwa vijana walioko shuleni.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi za kiafrika ambazo vijana wengi huanza matumizi ya pombe mapema katika umri mdogo. "Utafiti uliofanywa mwaka 2019 katika mikoa ya Mwanza na Kilimanjaro, ulibaini kuwa kiwango cha matumizi ya pombe miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari wenye umri wa miaka 15 na zaidi kilikuwa kati ya asilimia 12.9 kwa wasichana mkoani Mwanza hadi asilimia 63.9 kwa wavulana mkoani Kilimanjaro," alisema.

Alibainisha kuwa wakati kiwango cha matumizi ya pombe miongoni mwa wanafunzi wenye umri wa miaka 13 hadi 15, Mkoa wa Dar es Salaam kilikuwa asilimia asilimia 5.6.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa programu hiyo katika Shule ya Sekondari ya Msasani wilayani Moshi, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Obinna Anyalebechi alisema, "SBL inafurahi kusaidia uanzishwaji programu ya SMASHED dhidi ya unywaji pombe chini ya umri kwani inaimarisha shughuli za kuhakikisha bidhaa zetu haziuuzwi au kutumiwa na watu walio chini ya umri wa miaka 18.

Alisema programu hiyo inahusisha utoaji mafunzo muhimu kuhusu athari hasi za kunywa pombe chini ya umri kwa vijana na jamii kwa ujumla.

"Programu hii inachanganya matumizi ya maonesho ya maigizo na ushiriki wa wanafunzi katika mazingira ya kujifunza yanayowapa motisha ili kuwajengea uwezo.

"Pia kuwajengea ujuzi na ujasiri wa kufanya uamuzi wenye dhamira nzuri na kuendelea kuwa na mitazamo chanya ya kujali na kutunza afya zao," alisema.

Anyalebechi alisema SBL iliandaa programu hiyo miaka miwili iliyopita ikitoa elimu kwa wanafunzi walio chini ya umri katika mikoa ya Dar es Salaam na Tanga ambapo kampuni hiyo iliwafikia zaidi ya wanafunzi 20,000 katika mikoa hiyo.



Ofisa Msimamizi wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Joel Lema (kushoto), akitoa elimu ya kodi kwa mfanyabiashara Maryam Usanga katika eneo la Lovelosi, mkoani Arusha jana, wakati wa kampeni ya utoaji elimu ya mlango kwa mlango yenye lengo ya kuelimisha na kusikiliza changamoto na malalamiko mbalimbali kwa lengo kuboresha huduma za TRA. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapeana mbinu kuboresha usalama wa mahali pa kazi

**Na Halfani Chusi**

TAASISI inayojihusisha na usalama kazini ya TOHASA imekutanisha wadau kubadilishana ujuzi na kuboresha utendaji kazi.

Mkutano huo ulikutanisha wadau wa kampuni mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi jijini Dar es Salaam juzi.

Mkurugenzi wa Mafunzo, Utafiti, Takwimu na Uhamasishaji wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Joshua Matiko, aliutaja ni mkutano muhimu kwa kuwa umekutanisha wataalamu mbalimbali wa afya na usalama kazini na utakuwa na tija katika utendaji wa kazi wa ndani na nje ya nchi.

Akizungumza kwa niaba ya serikali katika mkutano huo, Matiko alisema serikali za nchi zote duniani zimejikita kwenye masuala ya usalama wa afya mahala pa kazi, hivyo kila mtu anapaswa kuzingatia hilo.

Mwenyekiti wa TOHASA, Caroline Balaza, alisema mkutano huo utaleta mafanikio kwa kuwa umekutanisha wataalamu na wafanyabiashara mbalimbali kubadilishana ujuzi na kutoka na jawabu la pamoja katika ajenda hiyo.

Caroline alisema kuwa awali ilikuwa ni ngumu kukutana na wadau kujadili pamoja lakini kwa sasa imewezekana na hayo ni mafanikio makubwa.

"Ninashauri serikali itambue wataalamu wa usalama wa afya pahali pa kazi, sera zikiboreshwa na wataalamu wakihusishwa, itasaidia kupiga hatua katika eneo hilo," alisema Caroline.

Meneja wa Afya na Usalama Kazini kutoka Mgodi wa Geita (GGML), Isaack Senya, ambaye pia ni miongoni mwa walioshiriki mkutano huo, alisisitiza muhimu wa kuzingatia afya za wafanyakazi.

Senya alisema mafunzo waliyopata pamoja na kubadilishana uzoefu na wataalamu kutoka kampuni nyingine, yatawasaisia kuboresha zaidi masuala ya afya pahali pa kazi katika ofisi zao.

Alisema wana zaidi ya miaka 10 bila kupata tukio la mfanyakazi kupoteza maisha akiwa kazini. Kutokana na mafunzo hayo, watapata mafanikio makubwa zaidi katika eneo hilo.

"Ninashauri kampuni nyingine kushiriki mafunzo haya ili kujua namna ya kulinda afya na usalama wa mfanyakazi pahali popote.

"Mfanyakazi anapoumia au kupoteza maisha akiwa kazini ni hasara kubwa kuanzia ngazi ya familia mpaka kwenye kampuni.

"Wale ambao hawajapata hii fursa wajue kulinda afya ya mfanyakazi ni matakwa ya kisheria, ni wajibu kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa na afya nzuri ili kutoa huduma kwa familia zao," alisema.

David Ongesa, Rais wa Usalama Mahali pa Kazi Kenya (WSPAK), ambaye pia ni miongoni mwa washiriki, alisema ni fahari kushiriki mafunzo akiwa Tanzania kwa kuwa yamemwongeza ujuzi wa kwenda kusaidia kuboresha atakaporejea nchini kwao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari ichukuliwe kukabili maafa yatokanayo na masika

**MAMLAKA** ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetoa utabiri wa mvua ya masika ambayo itaanza kunyesha wakati wowote kuanzia wiki inayoanza kesho katika maeneo mbalimbali ya nchi. Aidha, taarifa ya TMA iliyotolewa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Dk. Ladislaus Chang'a, ilisema katika baadhi ya maeneo, mvua hiyo itaanza wiki ya kwanza ya mwezi ujao na inatarajiwa kukoma ifikapo Mei, mwaka huu.

Katika taarifa hiyo iliyotolewa juzi, TMA ilisema mvua hiyo itanyesha kwa wastani wa juu, hali ambayo inaweza kusababisha madhara katika baadhi ya maeneo. Miongoni mwa madhara hayo ni maji kutuama katika maeneo anuai, sekta za uchukuzi kuathirika kwa kuwapo uwezekano wa kutokea uharibifu wa miundombinu hasa barabara na reli.

Sambamba na athari hizo, TMA pia kupitia utabiri huo, imeonya kuwa kunaweza kuibuka magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu katika baadhi ya maeneo, hivyo tahadhari inapaswa kuchukuliwa ikiwamo kuweka mazingira safi.

Pamoja na kuwapo kwa athari hizo hasi, Dk. Chang'a pia alisema kutakuwa na neema kutokana na mvua hizo hasa kujaa kwa mabwawa ya maji, hivyo kuongezeka kwa kina kwenye vyanzo hivyo ambavyo kwa sasa ni tegemeo kubwa la umeme nchini.

Kwa mantiki hiyo, mvua ya masika itakuwa na neema kwa nchi kunufaika katika uzalishaji na upatikanaji wa nishati. Hivi sasa nchi iko katika tatizo la mgawo wa umeme, huku sababu kubwa ikitajwa kuwa upungufu wa maji katika mabwawa ya kuzalishia nishati hiyo. Kwa hiyo, kujaa kwa maji kwenye mabwawa hayo kutapunguza kwa kiasi kikubwa mgawo wa umeme ambao unaiandama nchi na kusababisha shughuli mbalimbali za uzalishaji kusuasua.

Athari nyingine chanya, kwa mujibu wa TMA, ni kupungua kwa joto ambalo hivi sasa ni kali katika maeneo mbalimbali nchini. Joto hilo limesababisha baadhi ya watu kukumbwa na matatizo ya kiafya kama ambavyo imeelezwa katika vyombo mbalimbali vya habari pamoja na wataalamu wa afya.

Kutokana na kuwapo kwa taarifa hiyo ya utabiri wa hali ya hewa, ni vyema wananchi na taasisi mbalimbali za serikali na binafsi, kuchukua tahadhari ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. TMA imetoa utabiri huo wakati takribani mwezi mmoja sasa kulikuwa na athari kubwa kiafya, miundombinu kuharibika na baadhi ya watu kupoteza maisha kutokana na mvua ya vuli ambayo ilinyesha kuanzia Novemba, mwaka jana.

Wahenga wanasema mtu akiumwa na nyoka hata akiona unyasi anashtuka, hivyo hakuna budi kuchukua tahadhari dhidi ya majanga yanayoweza kusababishwa na mvua ya masika ambayo iko karibu kunyesha.

Moja ya athari kubwa zilizotajwa ni uharibifu wa miundombinu. Ni dhahiri kwamba baadhi ya barabara na njia za reli zinaweza kuathirika katika maeneo kadhaa nchini kutokana na mvua hiyo, hivyo tahadhari zichukuliwe mapema ili kuzuia majanga kutokea.


Mamlaka zilizopewa dhamana ya kusimamia miundombinu zikiongozwa na wizara za ujenzi na uchukuzi, Wakala wa Barabara (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) zichukue tahadhari mapema kabla maafa hayajatokea wakati mvua ikinyesha.

Wakati wa mvua ya vuli ilishuhudiwa maafa katika sehemu mbalimbali yakiwamo watu kupoteza maisha kutokana na nyumba kubomoka, madaraja kuvunjika na kusababisha mawasiliano kati ya sehemu moja na nyingine kukatika, maji kujaa na vyombo vya moto kusombwa. Hiyo ilikuwa wakati wa vuli, hivyo maafa kama hayo yanaweza kuwa makubwa zaidi kutokana na wingi wa mvua itakayonyesha.

Pia kuna uwezekano wa kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko, hivyo hadhari ichukuliwe kwa kuweka mazingira safi katika maeneo ya makazi ikiwamo kusafisha mifereji ya maji machafu yote hayo yanawezekana kama kila mtu ka nafasi yake atatimiza wajibu wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wanaoacha dawa za kulevya wangewezeshwa kiuchumi

**JITIHADA** mbalimbali zimekuwa zikifanyika za kusaidia vijana kujinasua katika janga la matumizi ya dawa za kulevya, huku baadhi yao wakifanikiwa kuachana na dawa hizo.

Kwa sasa yako makundi ya vijana ambao wanahudhuria katika hospitali mbalimbali kupata tiba ya methadone baada ya kuachana na dawa za kulevya, ili warejee katika hali yao ya kawaida.

Lakini pamoja na jitihada hizo zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa kupinga dawa za kulevya, bado kuna mazingira halijakaa sawa ambayo yanaweza kukwamisha jitihada hizo.

Hapa ninazungumzia vijana wanaoacha matumizi ya dawa la kulevya na kuanza kutumia methadone, lakini wanaendelea kuishia katika mazingira yaliyosababishwa wakajiingiza katika matumizi ya dawa hizo.

Kwa mazingira, huenda wapo ambao wamejikuta wakirudi kwenye uraibu, kitendo ambako wakati mwingine kinaweza kusababisha wakapoteza maisha au wakaendelea kuumia.

Kwa maoni yangu, ninadhani iko haja ya kuwabadilishia mazingira ya kuishi au kuwatafutia shughuli za kufanya ili wasiendelee kuwa tegemezi kwa wazazi wao ama ndugu zao.

Ikiwezekana kuwe na nyumba nyingi za kuishi waraibu, katika maeneo mbalimbali nchini, vilevile kuwe na mikakati itakayosaidia kuwafanya wasiendelee kukaa bali wajishughulishe.

Ninaungana mkono maoni ya Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la kuhudumia waraibu wa dawa za kulevya la Life & Hope Rehabilitation Organisation (LHRO), Al-Karim Bhanji, anayeshauri kuwapo kwa mikakati ambayo itawawezesha kiuchumi vijana wanaoachana na matumizi ya dawa hizo.

Bhanji alitoa ushauri mjini Bagamoyo mkoani Pwani juzi, katika mkutano wa uhamasishaji wa afya bora kwa waraibu wa dawa hizo unaotekelezwa na shirika hilo katika kata tano wilayani humo.

Kata zinazohusika katika mradi huo wa mwaka mmoja unaolenga pia kuwafanya waraibu kutambua haki zao za msingi kuwa ni Dunda, Magomeni, Nianjema, Kisutu, na Kiromo, huku wafadhili wakiwa ni U.S. Ambassador Fund for HIV/AIDS Relief (AFHR Grant) and Pepfar.

Kwa kawaiada, maendeleo ya nchi huletwa na vijana ambao hutegemewa kuwa taifa la baadaye, hivyo wanapotokea wengine wanajihusisha na matumizi ya dawa za kulevya, maana yake ni kuwa taifa bovu la baadaye.

Lakini pia wanapobahatika kuachana na dawa hizo, ni muhimu kuwawezesha kutorudi walikotoka, kwa kuwawekea mazingira rafiki hasa ya kujishughulisha na kazi mbalimbali.

Ninaamini kwamba katika makundi ya vijana wanaotumia au kuacha na dawa za kulevya, wanaweza kuwamo wasomi wenye fani mbalimbali, ambao wanaweza kusaidiwa kurudi katika fani zao.

Pamoja na hayo, suala la kuwapa elimu ya ujasiriamali na kuwapa mitaji ili wajishughulishe na biashara mbalimbali au kilimo cha bustani, ni jambo la muhimu, kwa ajili ya kuwafanya wajiongezee kipato.

Mazingira hayo yanaweza kuwa rafiki kwa wanaoacha uraibu na kuwa raia wema na msaada kwenye jamii inayowazunguka, kutokana na kwamba watakuwa na shughuli za kufanya na kuepuka udokozi.

Kwa sasa kuna kundi kubwa la vijana 744 ambao wameacha matumizi ya dawa za kulevya wilayani Bagamoyo, ninadhani ni vyema wawekewe mazingira yatakayowafanya waendelee na mabadiliko hayo.

Ninaamini idadi hiyo ni kubwa, hivyo wakiwa na shughuli ya kufanya, wilaya itakuwa imepata kundi kubwa la vijana wanaojiingizia kipato, lakinia kulipa ushuru au kodi ya serikali kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Vijana hao walioachana na matumizi ya dawa za kulevya, wangepewa uzito ili wasiendelee kuingiza hasara kwa kulishwa au kugeuka kuwa wezi wa vitu vya nyumbani na kwenda kuuza.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Aliokoa maisha, alipenda watu na watu walimpenda



Pascal Mayalla

KWA wasomaji wapya, huu ni mwendelezo wa nilivyokutana na Edward Lowassa nikihusisha visa na mikasa ya hapa na pale.

Wiki iliyopita tuliishia nikiwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), umekuja mwaliko wa Wiki ya Maji, nikafanya mipango ili nipate ile safari. Ofisi haina mtu wa kamera, nikabeba kamera yangu, kufika eneo la tukio, nikafanya mambo fulani ambayo siyo.

Taarifa za jambo zikatua ofisini, kwenye fomu zangu za tathmini ya utendaji kazi (OPRAS) zikachafuliwa. Nikalazimishwa kutia saini, nikagoma. Kilichofuata baadaye ni barua ya kufukuzwa kazi kwa kosa la 'insubordination', nikaaga TBC.

Somo hapa ni kwamba mtu unaweza kutenda kitendo kidogo tu cha tamaa ya pesa ili kuvuta pesa mbuzi kikaja kukugharimu kwenye taaluma yako au kwenya maisha yako.

Baada ya kisa hicho, mimi na familia yangu tuliamua kuhama nchi, nikaanzia Uingezera na baadaye Marekani na familia ikakaa huko. Nikawa nahanja hanja kutafuta wapi haswa kuna maisha mazuri. Nikajaribu Sweden, Ujerumani, Uholanzi, Uswisi, nikatua Italia. Kote nilikopita nilijichanganya na Watanzania na bado na nikiwa na kitambulisho changu cha mwandishi wa habari (Press Card) ili kupata fursa ya kuingia kwenye tukio lolote.

Nikiwa Rome, Italia kukafanyika mkutano wa Kimataifa wa Siku ya Chakula Duniani Miaka 10 baadaye. Katika mkutano huo, Tanzania ilituma ujumbe mzito na mimi nikajiandikisha kama mwandishi wa habari kutoka Tanzania.

Siku ya mwisho ya mkutano, sijui nini hasa kilichotokea kwangu mpaka kesho.

Nikiwa kwenye eneo lilotengwa kwa ajili ya waandishi wa habari, nikiwa na kompyuta yangu, kamera na begi, nilitoka.

Ile kuzinduka tu, niko hospitali moja kubwa ya Rome, nimezungukwa na kundi kubwa la watu. Edward Lowassa, Profesa Anna Tibaijuka (wote mawaziri) na Balozi wa Tanzania nchini Italia kwa wakati huo, Profesa Costa Ricky Mahalu. Hapo ndipo naelezwa kuwa nikiwa chumba cha waandishi, nilizimika ghafla nikaanguka, nikakimbizwa hospitalini. Kadi yangu ya utambulisho ikaonyesha ni Mtanzania, ubalozi wakaarifiwa ndicho kisa cha kuzungukwa vile.

Hapo Hospitali nimepatiwa tu huduma ya kwanza, sikuwa na bima ya safari wala sikuwa katika ujumbe wa Tanzania. Nikaulizwa hali yangu, nikajibu najisikia vizuri tu. Natakiwa kufanyiwa uchunguzi wa kina lakini sina bima.

Lowassa akamwuliza Balozi Mahalu ubalozi unaweza kusaidiaje? Balozi akamjibu kwa kawaida ubalozi unasaidia watumishi wa umma tu tena walioko katika safari ya kikazi. Akasema mimi si mtumishi wa umma na hapo Rome niko kivyangu tu!

Ndipo Lowassa akasema huyu Mayalla japo si mtumishi wa serikali, ni Mtanzania mwenzetu, tunamfahamu, tena kile kipindi chake cha Kiti Moto, nilikuwa nakipenda sana, sijui kwa nini kilikufa?

Watanzania ni watu wenye upendo sana wawapo ughaibuni, Lowassa alianzisha harambee ya papo kwa papo, na ubalozi wetu Rome, ukatia mkono, ukaingilia kati kuanzia vipimo, bili yote ya hospitali, nikapimwa nikatibiwa nikaokolewa maisha yangu!.

Somo hapa Watanzania tuwapo ughaibuni. Tujenge utamaduni wa kujitambulisha ubalozini kwa ajili ya chochote kinachoweza kujitokeza. Pia ubalozi uwe na taarifa zako. Kilichoniokoa Italia ni kile kibali cha uandishi na nilipata msaada kwa hisani tu ya Lowassa. Lakini endapo ningejitambulisha ubalozini, nikakutwa na jambo kama lile ningesaidiwa kwa urahisi.

### HARUSI YA BINTI LOWASSA

Wakati Lowassa akiwa Waziri Mkuu alioza binti, Binti Lowassa, na mimi nilitafutwa kuwa MC wa tukio lile. Serikali nzima ilihudhuria na ikatokea tukawa marafiki na Bwana Harusi.

Kuanzia hapo, mimi nikawa mtu wa Lowassa. Hata kashfa ya Richmond ilipoibuka, bado nilisimama na Lowassa na kumuunga mkono hata katika harakati zake za kisiasa, ikiwamo ile Safari ya Matumaini.

Kuna msemo kwamba rafiki wa kweli ni yule akufaaye wakati wa dhiki. Wakati Lowassa anaugua, yale makundi ya watu hayakuonekana tena. Hata lile kundi la Friends of Lowassa, nimekuja kuliona msibani. Waliokuwa wanahangaika naye ni mkewe, watoto na familia na marafiki wachache pamoja na serikali kumhudumia kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni.

### SOMO KIFO CHA LOWASSA

Somo Kuu la kwanza la kifo cha mwamba huyu ni kijifunza kuweka akiba ya maneno. Nikisikiliza baadhi ya kauli za wanasiasa jinsi walivyokuwa wanamsema vibaya Lowassa akiwa hai, na sasa wamekuja msibani na kugeuza maneno bila aibu, naona hapa kuna funzo. Tujifunze kuweka akiba ya maneno na wakati mwingine ni bora kunyamaza kimya.

Somo la pili ni kuwa na dhamira. Ukidhamiria jambo lako lishikilie, usikubali kukatishwa tamaa. Lowassa alikuwa mtu mwenye maono na dhamira ya dhati.

Somo la tatu ni Lowassa ni mwalimu mkubwa wa siasa za kuwa na kiasi. Alikuwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), akafanyiwa figisu akakatwa kwa figusu, akahamia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Akiwa CHADEMA hakuisema vibaya CCM na aliposhindwana na CHADEMA na kurejea CCM, Lowassa hakuisema vibaya CHADEMA. Ni wanasiasa wachache sana wana haiba ya namna hii. Kwenye msiba wa Lowassa, CCM na CHADEMA wakashindana kumuenzi kwa kumzungumza kwa wema.

Pumzika Lowassa Pumzika. Ulikuwa mtu miongoni mwa watu na ukawatumikia watu kwa uwezo wako wote kwa kushirikiana na watu. Ukautoa uhai wako kwa ajili ya watu wako. Kwa kifupi ni kwamba Lowassa ametufia. Mwendo umeumaliza, imani umeilinda

**Bwana Alileta, Bwana Ametwaa, Jina lake Lihimidiwe....**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mungu tusaidie kwenye umeme, sukari na maji



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

HEBU mpenzi msomaji wangu, siku moja uende nyumbani kwa mwalimu na ukitoka hapo uende nyumbani kwa mbunge, utaona tofauti kubwa zilizopo.

Ukienda nyumbani kwa mwalimu, atakupokea kwa bashasha na utamwona akitoka nje na viti viwili, kimoja chake na kingine chako mgeni wake na atatafuta kivuli cha mti mkae.

Akishakusalimia au mkishasalimiana, atapenda kujua hali za wanao na hasa kujua afya zao, wanaendeleaje kimasomo na kama wana matatizo yoyote Ingawa anaweza asiwe na jinsi ya kuwasaidia.

Hakika atafurahia sana kukuona na kukudadisi mambo mengi zaidi yakiwa ni pamoja na yanayohusu maisha yenu na yeye hapo mnapoishi na hata kama umetoka mbali atapenda kujua ya utokako.

Nenda kwa mbunge, kwanza siye atakayekupokea. Utapokewa na ama msaidizi wake au watoto watakaokuwapo nyumbani wakati unawasili. Si ajabu hata asikuchangamkie wala kukuonyesha tabasamu.

Hatatoka nje na kiti bali atabaki ndani mpaka uingizwe na waliokupokea na kama atakuwa sebuleni atakukaribisha. Kama yuko chumba cha kulala itabidi ukae umsubiri.

Kama mnafahamiana kabla, utasikia anakuuliza "oh kumbe ni wewe!" Lakini kama hamfahamiani, utasikia anakwambia "enhe kuna shida?" Hapo itategemea umefuata nini. kama ni shida utamwambia lakini kama ni salamu tu, utajiju.

Kwa shida iliyokupeleka utapewa ahadi kuwa atawasiliana na fulani au fulani ili kuona kama utasaidiwa au la. Kama ni salamu tu, atakwambia yuko salama na anaendelea na majukumu kama kawaida ya kumsaidia Mama.

Mwalimu baada ya mazungumzo yenu, nakwambia atakusindikiza mpaka nje ya lango kama lipo au atakufikisha barabarani lakini huku kwa mbunge, utaagiwa sebuleni na kujiondokea huku ukisindikizwa kwa macho na waliokupokea.

Ukweli hii ndiyo hali halisi ya tunavyoishi Watanzania. Ndivyo tunavyoishi na wanasiasa wetu ambao kabla hawajawa wanasiasa, huwa kama walimu, lakini wakishapata huanza 'kubeba vyuma'.

Ni kawaida nyakati kabla ya uchaguzi na hasa unapokaribia kama ilivyo sasa, utaona jinsi watu wanavyonyenyekea, husan wanaowania kuweka nia.

Wakishachaguliwa tu, wanakuwa si wao tena, wanaanza kuwaza mengine kabisa.

Siku hizi mtu akichaguliwa au kuteuliwa, hubadilika na kuangalia ni nini atakipata kwa ajili yake na familia yake na watu wake wa karibu, hivyo kusahau waliojilawa vituoni kupiga kura.

Ndiyo sababu tunaona jinsi tunavyopitia vipindi vigumu kimaisha hivi sasa nchini. Umeme hauna uhakika, maji hayana uhakika, sukari ndiyo usiseme, lakini pia hata dola ya Marekani nayo ni adimu.

Tatizo ni nini? Watu wanajali matumbo yao, hawashughuliki na matumbo ya wengine. Wananchi wanapewa ahadi za uongo huku wakiendelea kuumia. Ile njoo kesho njoo kesho iliyokuwa ofisini imegeukia maishani.

Huyu anakwamba mgawo wa umeme utakwisha siku fulani, huyu anaibuka na kusema siku yake na mwingine hivyo hivyo lakini wa mwisho anakwambia tunaongeza miezi sita mgawo kwisha.

Wote hao ukiwatazama ni wabunge na wengine mawaziri. Wanatupokea wananchi wao sebuleni wao wakiwa vyumbani, tofauti na ambapo wangetoka nje na viti viwili tukakaa chini ya mti kuyazungumza na kuona tunakwendaje.

Unajiuliza hivi uchaguzi ungeitishwa leo hii, kweli wabunge wangerudi hawa hawa? Kwa sababu maumivu waliyo nayo Watanzania si ya dunia hii. Kama hakuna sukari lakini mwingine anaibuka, badala ya kukupunguza machungu anakwambia achana nayo utaugua, unafanyaje?

Anakwambia hivyo huku yeye tangu utoto amekua akinywa uji wenye sukari. Anakwambia hivyo wakati nyumbani kwake ana magunia ya sukari na hajui yalikotoka! Anataka uache sukari eti ni hatari wakati yeye anafakamia chai yenye sukari.

Kwa kweli maisha ya watu yanachezewa na kutiwa majaribuni na watendaji wetu, ambao naamini wakinyimwa mishahara watahaha, huku wakijua kuwa asiyefanya kazi na asile!

Alizoea kusema sana hayati John Magufuli, almaarufu kaka JPM na tutamkumbuka kwa kweli.

Ni kama alivyosema Mwenezi, Chifu Bagolole, mbona enzi za Jiwe hali ya kukatika umeme na maji haikuwapo? Mbona sukari haikupata kupotea hivi na hata kuuzwa sawa na kilo ya nyama? Ni kitu gani kimebadilika?

Kwa kweli Watanzania tunapaswa kujiuliza tulikosea wapi miaka takriban tisa iliyopita, mpaka tunajikuta katika lindi la matatizo kama hili na kujuta wenyewe sasa? Uchaguzi ujao tukifanya makosa, tutajizika wenyewe! Mungu endelea kutusimamia waja wako!

# ABU:
# Mbinu mpya kuandaa wafanyakazi wa baadaye

**Na Maria Seme**

KILIO cha wahitimu wa vyuo mbalimbali nchini kutokuwa na ubora kimeendelea kusikika. Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML), imepata suluhisho.

GGML, mdau mashuhuri katika tasnia ya madini nchini kwa zaidi ya miongo miwili, imekuwa mstari wa mbele katika kushughulikia suala muhimu la uhaba wa ujuzi na ukuzaji vipaji ndani ya sekta hiyo.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000, kampuni hiyo haijazingatia tu ubora wa utendaji kazi, bali pia kuwekeza katika nguvu kazi ya baadaye ya Tanzania.

Kwa kutambua umuhimu wa kuandaa wafanyakazi wa baadaye na kukuza vipaji, GGML kwa kushirikiana na wadau wengine, ilitoa mchango mkubwa wa zaidi ya Dola za Marekani milioni mbili mwaka 2009 katika kuandaa mitaala ya kuandaa vijana wa kitanzania kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Moshi.

Mpango huo umezaa matunda kwa miaka mingi, zaidi ya vijana 1,400 wamepata mafunzo ya uchimbaji wa kina kifupi juu ya ardhi, hivyo kusaidia kupunguza uhaba wa ujuzi katika sekta hiyo.

Hata hivyo, dhamira ya GGML katika kukuza vipaji inazidi mafunzo ya ufundi stadi. Mnamo 2009, kampuni ilizindua mpango wa kuajiri wahitimu ili kutoa fursa za mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu wa vyuo vikuu wasio na ajira.

Programu hiyo ilikuwa na idadi ya wahitimu 12 kila mwaka hadi mwaka 2012. Baada ya kusitishwa kwa miaka mitano, GGML ya 2017 ilirejesha programu ya mafunzo kwa vitendo, ikiwapa vijana wa kitanzania uzoefu muhimu wa kufanya kazi ndani ya GGML kwa mwaka, huku ikiwaruhusu kubobea zaidi katika fani zao.

Kati ya 2017 na 2023, GGML ilichukua wahitimu 194 kwenye programu yake ya mafunzo tarajali.

Katika kupanua mafunzo hayo, mwaka huu, kampuni hiyo imekuja na programu iliyopewa jina la African Business Unit (ABU) ambayo ni zaidi ya program ya mafunzo taraji yanayotolewa kwa mwaka.

Katika progamu hiyo ya ABU, jumla ya wahitimu 10 wa mafunzo tarajali kwa mwaka jana wamechaguliwa kuendelea na programu hiyo ambayo mbali na kupata mafunzo ya juu zaidi, pia wamepata ajira za kudumu ndani ya GGML.

Menejea Mwandamizi wa Masuala ya Rasilimali watu, Charles Masubi anasema dhumuni la kuwa na mafunzo hayo tarajali kwa wahitimu wa vyuo vikuu kwanza ni kushirikiana na serikali kuhakikisha wahitimu wanapata ujuzi stahiki.

"Lakini, kwetu sisi GGML ina maana kubwa zaidi ya hapo kwani tunaandaa wafanyakazi wetu wa baadaye tunatengeneza vipaji ambavyo huwa tunavichukua baada ya kuvinoa kutoka kwa wahitimu na kuwaajiri.

"Mbali na kuwafundisha kwa mwaka mmoja, pia tunawapatia kila maarifa wanayohitaji kwenye eneo lao la utaalamu kama ni mhandisi tunahakikisha tunamfundisha na kumpa maarifa yote kwa vitendo akisimamiwa na wahandisi wabobevu," anasema.

Masubi anasema programu hiyo ya ABU inawajumuisha wahitimu wa vyuo mbalimbali waliomaliza progamu ya mafunzo tarajali kwa mwaka mmoja ndani ya GGML.

Hii ina maana kuwa baada ya kumaliza mafunzo hayo tarajali wahitimu waliofanya vizuri wanaunganishwa na waliopo kwenye migodi mingine ya Afrika ambapo wanafanya programu kama hiyo ya GGML.

"Kisha tunawapa mafunzo ya juu zaidi ya ujuzi au juu ya elimu yao ya darasani, kama ni mhandisi tutamfundisha kuweka vipaumbele, makubaliano, kuandaa bajeti kupata ujuzi wa namna ya kuwasiliana kwa usahihi na wenzake. Kwa sababu vyote hivyo ni muhimu katika kufanya kazi," anasema Masubi.

Anasema waashiriki wa programu hiyo watashirikiana na migodi ya Afrika iliyo chini ya kampuni mama ya AngloGold Ashanti kwenye nchi za Ghana na Guinea.

"Wote watakuwa kwenye programu inayofanana na lakini bado wakiendelea kubobea zaidi kwenye fani zao na kufanya mzunguko wa kujifunza zaidi kwenye migodi mingine.

"Hawa watu hatuwaandai kuishia kuwa wafanyakazi wa ngazi za chini, wakati mwingine tunawaandalia fursa ya kupanda juu na kuwa viongozi wakubwa wa kampuni hapo baadaye.

"Tunapokuwa na programu ya pamoja tunatengeneza kiongozi ambaye atafahamu mila na desturi zetu za kazi kama kampuni, utamaduni wetu wa kazi, miiko yetu kila kitu kuhusu kampuni kwa hiyo ikitokea kiongozi huyu amepata nafasi kufanya kazi Ghana atakuwa na ufahamu wa kutosha.

"Atakwenda akiwa ameiva kwenye nyanja zote tunazozingatia AngloGold Ashanti mfano masuala ya uhasibu, uhandisi, mawasiliano, lazima awe vizuri kwa hiyo anakuwa mtaalam ambaye anaweza kuwa kwenye idara yoyote na kufanya kazi vizuri na kukua. Hilo ndio lengo kubwa la kuanzishwa kwa ABU," anasema Masubi.

Mmoja wa wahitimu hao ni Diana Laswai ambaye mbali na kuishukuru GGML pia waliishukuru serikali kwa kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kutoa mafunzo kazini kwa vitendo.

Pia alitoa wito kwa wanafunzi wapya wanaoanza mafunzo hayo mwaka huu kufanya kazi kwa bidii, kuzingatia nidhamu na kuzingatia tunu za GGML ambavyo ni usalama.

Evelyne Julius ambaye ni mhandisi wa masuala ya umeme, anayesema, "Nimejifunza vitu vingi. Kuwapo kwangu GGML ni fursa ya kipekee kwa sababu nitaweza kutekeleza miradi mbalimbali kwa ujasiri na ujuzi nilioupata," anasema.

Mkunde Frank ambaye ni mteknolojia wa masuala ya jiolojia, anasema nafasi aliyoipata ya kuendelea kufanya kazi ndani ya GGML kupitia progamu ya ABU, imeendelea kumjengea kujiamini na kunoa zaidi ujuzi wake.

"Mathalani kwenye kitengo cha geolojia tumepata fursa ya kipekee, kila mfanyakazi anapewa uthamani bila kujali mkubwa au mdogo.

"Lakini hata ukishuka kwenye machimbo chini ya ardhi kila mfanyakazi anazingatia mafunzo aliyopewa kwa vitendo hasa katika kutekeleza kipaumbele cha kwanza ambacho ni usalama," anasema.

Mkuu wa Idara ya Mafunzo na Ujuzi kutoka Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Albert Rukeisa anasema jitihada hizo za GGML kwa zaidi ya miaka 15 zimekuwa chachu kwa waajiri wengine kuendelea kutoa nafasi kwa vijana kujifunza na kuongeza wataalam wa madini katika sekta hiyo.



Meneja Mwandamizi wa Masuala ya Rasilimali Watu kutoka GGML, Charles Masubi (kulia) akisalimiana na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigella (kushoto) wakati wa uzinduzi wa programu ya mafunzo tarajali ya GGML kwa 2024/25. Katikati yao ni Makamu wa Rais Mwandamizi wa AngloGold Ashanti - Kitengo cha Ubia na Ushirika Afrika kutoka AngloGold Ashant - GGML, Terry Strong na Katibu Mtendaji wa Chemba ya Migodi Tanzania, Benjamin Mchwampaka.



Wahitimu 40 wa vyuo mbalimbali nchini ambao wanatarajiwa kuanza mpango wa mafunzo kazini kwa vitendo unaodhaminiwa na GGML kwa mwaka 2024/25 wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kukaribishwa rasmi mwishoni mwa wiki mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPI-**

# MAISHA

FEBRUARI 25, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 14


## Saladi ya limao na vitunguu




## Mtindi unavyong'arisha uso

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | U | R | A | I | A |
| W | | | | I | | N |
| A | | D | O | M | | G |
| L | O | A | | B | U | U |
| I | | I | L | E | | K |
| M | | M | | | | I |
| U | K | A | M | E | | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

NOA, ANA, BAO, TEE, PUNJE, BANDA, NYOTA, AMANI, UBWABWA, ENDELEA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

3 5 8 7 5 8 5 A 4 9 0
9 6 9 6 7 9 4 3 8 0 8
5 8 5 8 5 8 7 C 9 0 2
1 I 9 8 9 4 8 9 4 4 8 9
5 9 6 8 2 8 1 3 8 5 8
3 8 9 4 8 H 8 8 0 3 3
8 5 9 4 8 0 8 0 3 8 2




## WATOTO

# PAKA RANGI







MZUNGU mmoja alionekana kumdharau Mbongo, akamwambia waulizane maswali na akishindwa anampatia Sh. 5000 na endapo yeye atashindwa atatoa 100,000.

**Mzungu:** Nchi ipi ilishindwa kwenye vita kuu ya kwanza ya Dunia?

**Mbongo:** akashindwa akatoa 5000 kuashiria hajui.

**Mbongo:** Kitu gani kikienda juu kina miguu minne na kikirudi chini kina miguu mitatu?

**Mzungu:** akafikiria akakosa jibu akatoa 100, 000, kuashiria hajui ila akataka kujua, akauliza ni nini hicho?

**Mbongo:** Akatoa 5000 kuashiria hata yeye hajui!.

**SWALI**

Samaki aina ya Pweza ana mikia mingapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Ulimwacha mke, sasa unataka akurudie kama kimada!

MPENZI msomaji, tunaendelea kumulika yaliyojificha kwenye ndoa nyingi. Wako baadhi ya kinababa huanzisha mitafaruku, baadaye wanaweka mikono kichwani!

Wako pia kinamama hukimbia manyanyaso na kuolewa kwingine na mume kuoa mwingine. Vyanzo vya mitafaruku ni vingi na havivumiliki.

Mume anaweza kuwa amepata mwanamke mwingine nje ya ndoa, hivyo kumnyanyasa mkewe wa ndoa ili kumfanya aghadhabike na kujiondokea zake. Inapotokea hivyo, kuna baadhi ya kinababa hufurahia ili huyo mwingine azibe nafasi. Huu ni usaliti ambao hata Mungu haupendi.

Kwanza, nianze na mume aliyeacha mke. Juzi nikiwa nasikiliza redio moja alfajiri, msikilizaji mmoja akamwuliza mtangazaji, je, ni haki?

Yuko jamaa mmoja alimwacha mkewe na kwenda kuoa mwanamke mwingine. Mambo yakamchachia akamrudia mkewe wa kwanza kumwomba warudiane, lakini kama kimada wake.

Mpenzi msomaji, alipotamka hilo la kimada nikajikuta nimecheka kwa sauti kubwa na mtangazaji naye akacheka. Ulimwacha, sasa umedata unataka awe kimada wako? Jamani! Ama kweli Maisha ndivyo Yalivyo.

Kituko kingine, yuko baba alifiwa na mkewe. Kabla ya kifo walikuwa wametengana, huyu akaoa na yule akaolewa kwingine.

Kabla ya kufarakana tayari walikuwa na watoto wakubwa watatu, mkubwa akiwa tayari ameanza kujitegemea na ameshajenga nyumba yake ndogo ya vyumba viwili. Pale msibani ndipo mambo yakabumbuluka.

Kwanza, muda mwingi baba wa watoto hao alikuwa kajiinamia akionekana kuwa na mawazo mazito. Alichokuwa anawaza anakijua mwenyewe. Mkewe hakuzikwa kijijini kwake wala mama mkwe hakuja msibani.

Kwenye kikao pale msibani, watoto walihoji mbona baba yao aliwatelekeza kwa takribani miaka minane bila kujua wanaishi vipi? Wakahoji hata kama alikuwa na mwanamke mwingine mbona hajawatambulisha wamjue?

Baba akajitetea kutowatelekeza na kwamba anawapenda sana. Akaambiwa na kikao cha familia kwamba anatakiwa akafanyiwe usuluhishi nyumbani kijijini ili kupatanishwa na watoto wake.

Hata hivyo, watoto wakaibua dai lingine wakitaka baba yao kama kweli anawakubali ni watoto wake, ahame kwa huyo mwanamke aje akae nao. Yule mtoto mkubwa (wa kiume) mwenye nyumba akamwambia baba yake anamruhusu aje akae hapo nyumbani kwake lakini siyo na huyo mwanamke (wajumbe wa kikao wakaangua kicheko).

Mtoto mwingine wa kike akainuka na kusema kama baba yao hataki kuja kuishi nao, basi baba yao apange zamu ya kukaa nao yaani kama wiki hii ataishi nao basi wiki ijayo akaishi na huyo mwingine (Wajumbe wa kikao wakaangua tena kicheko).

Mpenzi msomaji, ijapokuwa kilikuwa kikao cha kuanua tanga ambacho nami nilishiriki, ilikuwa burudani ya aina fulani. Kwa ujumla, baba yule alipata aibu kubwa.

Kwa baba anayeithamini familia yake na kuwajibika vilivyo, hakupaswa kuwasahau watoto wake hata kama ametengana na mama yao. Alipaswa kuwa karibu nao kwa kuwa ndiyo baraka na hazina aliyompa Mwenyezi Mungu.

Angalia mke aliyemzalia watoto wazuri, wenye akili na mkubwa ameshajenga nyumba yake ambako ndiko walikokuwa wakimwuguzia mama yao na baba mwenyewe hajafanikiwa hata kuwa na kibanda, amepanga.

Mtoto huyo mkubwa wa kiume alitamka wazi kuwa yuko radhi kumwachia baba yake nyumba ile ikiwa atarudi kuishi hapo lakini kwa sharti kwamba asimlete pale mwanamke wake huyo. Sharti hilo baba huyo alilikataa kwa madai eti tayari amezaa na mwanamke huyo, hivyo hawezi kukaa mbali naye.

Hata ile ofa ya kuja kukaa na wanawe kwa wiki kisha aende tena kwa mkewe huyo hakuiafiki. Kikao kikaamua kuwa majibu zaidi ya maswali hayo yatapatikana wakati watoto hao watakapokwenda kijijini ambako kikao cha ukoo kitafanyika.

Mpenzi msomaji, hayo ndiyo mambo ndani ya nyingi ya familia. Usione watu barabarani wakitabasamu kumbe wamebeba mizigo mizito vichwani na nafsini mwao. Hakika Maisha Ndivyo Yalivyo.

Mpenzi msomaji wangu, bila shaka umepata picha ya kile nilichotaka kukushirikisha katika makala ya leo. Mke wa awali ni mkeo tu hata kama yule wa pili utamwona kama lulu. Isitoshe, watoto wa awali kwenye ndoa yako ni ufunguo wa baraka katika maisha yako, hivyo hapaswi kuwapuuza au kuwatelekeza. Wakimlilia Mungu, adhabu yake utaionja hapa duniani.

**Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe kupitia 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Ndoa haianzi kama ajali, chungulia ramani kwanza

LEO nataka tuzungumze pamoja mambo mawili kuhusu misingi ya ndoa, na kutazama faida au hasara zake. Mpango wa Mungu wa ndoa, ni sawa na ramani.

Sote tunajua kwamba ramani ni mchoro wa kitaalamu unaoonyesha kitu fulani, iwe nyumba, kiwanja au miji, maliasili au barabara.

Ninachotaka tuweke maanani, ni barabara zinazokuwezesha kufika sehemu uliyokusudia. Kwa kufuata ramani, itakuonyesha vituo utakavyopitia. Ukipuuza kufuata ramani, kwa kujifanya mjuaji, utapotea hakika. Hutafanikiwa kufika uendako.

Mungu kwa kutaka wote tufikie ndoa yenye amani, upendo, furaha, ushirika na umoja, aliweka utaratibu wake wenye vituo vitatu.

Katika kitabu cha Mwanzo: 2: 24, maandiko matakatifu yanasema, “Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake, naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.”

Kwa andiko hilo, tujadili ninavyoviita vituo vitatu. Mosi, kuacha (kuondoka), kuambatana na kuwa mwili mmoja. Ramani yetu inatutaka tutoke kituo cha kwanza, twende cha pili, ndipo tumalizie cha tatu.

Anza kwa maandalizi. Ni lazima ujue kwamba ndoa huwa haianzi kama ajali. Yaani unaamka asubuhi, unakutana na kijana, na kesho yake uko kwenye ndoa. Tena haitokei kama mvua za El-Nino. Yaani haikutarajiwa, imetokea tu, hapana!

Ndoa inaanza na mipango na kufuata taratibu zinazokubalika katika serikali, jamii na kanisa. Uhusiano huanzia kwenye urafiki. Urafiki ukikomaa, huzaa uchumba.

Uchumba si kipindi cha kumweka mwenzako kwenye vipimo au majaribio; ni kipindi ambacho kila mmoja ana uhakika asilimia 100 kwamba huyo aliye naye ndiye chaguo sahihi alilopewa na Mungu. Hii ndiyo inayompa kijana ujasiri wa kuwashirikisha wazazi, kanisa na jamii kwamba wako kwenye agano la kweli la uaminifu, lenye lengo la kuingia katika ndoa takatifu.

Ukiamua kuondoka, ondoka kimoja. Baada ya kufuata taratibu zote, sasa unafika wakati wazazi pamoja na jamii husika, wanawaruhusu kwa baraka zote vijana wao kufunga ndoa takatifu.

Familia nyingi za kiafrika huanza kwa kumuaga binti rasmi, kwenye ibada na sherehe, Maarufu kwa jina la ‘sendoff’. Biblia inatupa mfano hai wa tendo hili.

Angalia na soma kitabu cha Mwanzo: 24:50 kinasema hivi: “Ndipo Labani na Bethueli wakajibu wakasema, neno hili limetoka kwa Bwana, wala sisi hatuwezi kukuambia neno jema wala baya. Tazama, huyo Rebeka yuko mbele yako, umchukue, ukaende zako awe mke wa mwana wa bwana wako, kama alivyosema Bwana.

Inamalizia kwa kusema, “Wakambarikia Rebeka wakamwambia, Ndugu yetu, uwe wewe mama wa kumi elfu, mara elfu nyingi, na wazao wako waurithi mlango wa hao wawachukiao. Rebeka akaondoka na wajakazi wake, nao wakapanda juu ya ngamia wakamfuata yule mtu.

Kuna jambo la kujifunza hapa. Hii ni habari ya binti Rebeka aliyeolewa na mwana wa Ibrahimu, Isaka. Baada ya mjumbe (leo tungemwita mshenga) kupewa ruhusa ya kuondoka naye, sikia kilichoendelea.

“Kisha huyo mtumishi akatoa vyombo vya fedha, na vyombo vya dhahabu, na mavazi akampa Rebeka; na vitu vya thamani akampa nduguye na mamaye pia. Wakala, wakanywa, yeye na watu waliokuwa pamoja naye, nao wakakaa usiku. Wakaondoka asubuhi.”

Kwa hiyo uchumba si jambo la sirini. Mambo yote yanafanyika wazi tena mbele ya mashahidi. Ni aibu, tena fedheha vijana kujioza wenyewe, kwa kisingizio chochote, na hasa vijana wanaoishi mijini.

Kuna kundi la wanandoa ambao wameishi kwenye mahusiano hayo kwa muda mrefu pasipo wazazi kuhusishwa au kutembelewa. Ukiwauliza wanakujibu, ‘bado tunapimana’ na wana watoto tayari.

Au ‘bado tunajiandaa’, yaani wanajianda kuoana na wameshaoana. Kama wewe msomaji ni katika kundi hilo, tengeneza mambo yako na wazazi, kanisa na Mungu, haraka.

Jambo la pili tunalikumbushwa hapa ni ule umuhimu wa kuwathamini wazazi wa binti na ndugu zake. Kumbuka mkeo sio kama uyoga pori, uliojiotea wenyewe tu.

Amelelewa na kukuzwa katika jamii fulani. Waonyeshe moyo wa shukrani kwa kuwapa chochote. Tunaona huyu mjumbe, baada ya kukabidhiwa binti, hakusema, ‘oh haleluya, sikudaiwa kitu’. Alijua na kutimiza wajibu wake.

Lingine hapa ni umuhimu wa wazazi na jamii husika kutoa baraka wa vijana wao. Sio kuwalaani kwa upungufu uliojitokeza bali kwa maneno ya heri na baraka.

Usiondoke kama mke wa Lutu. Kwa habari ya kuondoka inawahusu wote, mume na mke. Katika kizazi cha leo, wanawake wengi wanaogopa kuolewa.

Pamoja na sababu nyingine, wengi hawapendi kutawaliwa. Wanataka kujitawala. Mioyo yao inapiga kelele ikisema, ‘wanawake tunaweza’.

Wanaume nao wanaogopa kuoa. Pamoja na sababu nyingine, hawataki kuwajibika wala kushiriki mali na fedha zao na mwanamke mmoja tu. Hofu ziko pande zote.

Hii imesababisha watu kama hawa kuingia kwenye ndoa, mguu mmoja ndani ya ndoa na mwingine umewekwa mahali fulani, nje ya ndoa. Mke anaweza kuficha baadhi ya fedha au mali zake mahali pengine, labda kwa wazazi wake.

**• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# Send-off





ILI-KUWA siku ya furaha kwa ndugu, jamaa na marafiki wa Neema Japhet Hume wakati wakimuaga kwa ajili ya kwenda kuanza maisha mapya ya ndoa. Sherehe hiyo ilifanyika Novemba 26, mwaka jana katika ukumbi wa Lavender Hall Jijini Dodoma.





# MITINDO

# INATOSHA KUTOKA HIVI...



MAVAZI ni moja ya utambulisho na kutoa taswira inayotafsirika vyema kuhusu tabia, maisha na mapenzi ya mtu husika.

Katika kundi la vijana, wengi inatosha kutambuliwa kutokana na mavazi pekee. Hapo utamjua mtu uliyenaye wakati huo kama anaendana na wewe kwa kumuangalia tu.

Hata hivyo, idadi kubwa hawajui njia nzuri ya kuvaa , hivyo leo nitaeleza namna ya kupangilia nguo ili kukupa mwonekano mzuri.

Mazingira/sehemu

Kijana lazima ujue kubadilika kulingana na mazingira ya mahali unapotaka kwenda, kwani kila mahali kuna vazi lake rasmi .

Mfano ukienda ofisini hutakiwi kuvaa jezi au kwenye harusi kuvaa kaptula na fulana. Ni lazima utambue mavazi sahihi na mazingira unayotaka kwenda.

**VAZI LA PENSI**

Ukivaa kaptula au wengine wainata pensi, basi hakikisha unavaa soksi fupi zisizoonekana, miguuni pigilia raba au makubanzi na haipendezi mtindo wa kuchomekea.

**SHATI JEUPE**

Kama mpenzi wa mashati meupe, hakikisha rangi inakuwa ya kiutu uzima na sio kama sare za wanafunzi wa shule.Kama utapenda ubunifu vaa lenye urembo kiasi au limetengenezwa kwa mtindo wa kisasa zaidi.

**SURUALI NYEUSI**

Suruali nyeusi ni moja ya mavazi ambayo yanatakiwa asikose kuwa nayo kwa upande wa wanaume kwa sababu inaendana na kila aina ya nguo, pia inahimili uchafu.



URÉMBO

Na Mary Geofrey







# Mtindi unavyong'arisha uso

KUNA njia nyingi za kutibu chunusi katika sehemu mbalimbali za mwili hususani usoni.

Njia wanazotumia wengi ni kutumia mafuta na krimu zenye kemikali ambayo husababisha madhara.

Leo tutaeleza njia rahisi ya kuondoa chunusi kwa kutumia maziwa ya mtindi,asili,karoti, yai, jani la chai na mlozi.

**JINSI YA KUANDAA**

Chukua maziwa ya mtindi na utumie kusafisha uso wako kwa kusugua uso taratibu na ukimaliza fuata hatua zinazofuata.

Chukua mchanganyiko wa mlozi, karoti au jani la chai na anza kusugua usoni taratibu kwa dakika tano.

Ukimaliza safisha kwa kutumia maji ya uvuguvugu yaliochanganywa na kipande cha limao lililowekwa katika taulo la pamba.

Hakikisha unafuta uso wote kasoro kwenye tatizo.

Weka ute mweupe kwenye taulo lako na anza kujisugua taratibu kwenye uso wako.

Jisafishe na maji ya vuguvugu ili kuondoa ukavu wa ngozi, kata matango na yabandike katika ngozi na fanya hivyo mara tatu kwa wiki utaanza kuona matokeo mazuri.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Saladi ya limao na vitunguu



SALADI ya limao na vitunguu ni chakula maarufu ambacho hutengenezwa kwa kutumia vitunguu maji vibichi vilivyo katwa katwa, limao iliyo kamuliwa, pamoja na viungo.

Saladi hii yafaa kula pamoja na chapati, pilau, biryani au wali wa aina yoyote.

Fuata hatua zifuatazo, ili ujifunze jinsi ya kutengeneza saladi hii ya limao na vitunguu.

**Namna ya kutengeneza**

Chukua kontena na weka vitunguu maji pamoja na chumvi, kisha changanya vizuri.

Funika vizuri kontena hilo na uliweke pembeni kwa muda wa saa mbili.

Baada ya hapo chukua chujio na uchuje maji yote ya vitunguu hivyo, kisha virudishe kwenye kontena.

Weka majani ya giligilani, limao, tangawizi, pamoja na vitunguu swaumu, halafu changanya vizuri, kisha funika vizuri kontena hilo na uliweke kwenye friji kwa muda wa saa 2 kabla ya kula.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Yajue haya kabla kuanza ujenzi wa nyumba

UJENZI wa nyumba ni uwekezaji kama ulivyo uwekezaji mwingine wowote.

Ni vigumu sana kufanikisha kuwa na nyumba ya ndoto yako endapo hujaweka mipango mizuri ya kuwekeza pesa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hiyo unayoitamani.

Mtaalamu wa ujenzi, Khamis Ally, anasema kuna vitu ambavyo mtu ambaye amekusudia kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba anapaswa kuvifahamu. Moja ya vitu hivyo, anasema ni kuweka mipango madhubuti juu ya ujenzi wa nyumba katika mtazamo wa sasa na wa baadaye.

"Unapopanga kujenga nyumba yako ni muhimu kuiona baadaye na mabadiliko yake. Ni vyema ujue jengo lako litakavyokuwa kabla ya kuanza ujenzi, ufahamu uzuri wake, ukubwa, kimo na rangi.

"Ujue ni wapi utakwenda kununua vifaa vya ujenzi kama saruji, mbao na nondo. Pia umfahamu fundi atakayekujengea, ukanda unaojenga ni wa aina gani kijiografia, kama eneo lako halina mgogoro wowote, iwe ni kwa upande wa serikali au majirani," anabainisha.

Jambo lingine ambalo mtaalamu huyu anashauri ni kujenga nyumba inayokidhi mahitaji yako.

Kwamba ni muhimu kufahamu ni nyumba ya aina gani unayotaka kujenga kwa kutazama mahitaji yako katika uhalisia wa sasa na wa baadaye na kumshirikisha mtaalamu aliyebobea katika usanifu wa nyumba za kuishi.



"Kujenga kwa kuzidi mahitaji yako kunaweza kuleta hasara kwa kushindwa kumaliza ujenzi. Unaweza ukajiuliza maswali kadhaa, Je, kuishi kwenye hiyo nyumba ni faida zaidi kuliko kupanga? Ni muhimu kuhakikisha kwamba unajenga kwa faida na si hasara.

"Baadhi wamejikuta wamejenga nyumba ambazo zinadumu kwa muda mfupi. Wako waliofikiri kutumia vifaa duni vyenye gharama ndogo ndiyo namna ya kupunguza gharama na badala yake walijikuta wakihitajika kuvibadili baada ya muda mfupi na kwa gharama kubwa zaidi," anasema.

Pia anasema wako pia waliochakachua kwa kujua kwamba ndio njia nzuri ya kupunguza gharama, na kujikuta katika hatari za nyufa, kubomoka na kutokudumu kwa muda unaofaa. Kwa mantiki hiyo, anasema mtu ahakikishe anakuwa na mtazamo wa kiuchumi wa kujenga kilicho bora, imara, kinachodumu na kwa gharama nafuu.

Ally anasema kabla ya kuanza ujenzi wa nyumba, ni vizuri pia kudodosa na kupata taarifa sahihi zinazohusiana na ujenzi zikiwamo gharama ambazo hutumika kulipa mafundi, vifaa vinavyopaswa kununuliwa ili kukusaidia kufanya uamuzi bila hofu na kutokuonekana hajui chochote mbele ya mafundi na wakatumia mwanya huo kumdanganya baadhi ya vitu.

Pia anashauri mtu kusimamia ipasavyo ujenzi wa nyumba yake kuanzia mwanzo hadi mwisho ili kuhakikisha kila kitu kinakwenda kama kilivyopangwa badala ya kuwaachia huru mafundi.

## DONDOO

# Zingatia haya kufurahia kibaraza chako

**Na Restuta James**

MAUA ni pambo la asili ukutani, viti vichache na meza ndogo nzuri ni vitu vitakavyokupa hamu ya kukaa kibarazani kwako.

Wataalamu wa mapambo wanaeleza kwamba hivi ni vitu vinavyonogesha mandhari ya kibaraza, kiwe kikubwa au kidogo.

Baadhi ya wataalamu kwenye mtandao wa Pinterest, wanasema matumizi ya vitu vya asili katika eneo hilo yakiwamo maua kunaongeza hewa na utulivu.

Wanasema 'visosi' au nyungo vilivyofumwa kwa ukili na kunakshiwa kwa rangi tulivu ni pambo tosha kibarazani.


"Panapendeza sana ukiweka meza ndogo ya mbao, unaweza kujenga mazoea ya kunywa kahawa kibarazani au kupumzika ukisoma kitabu cha riwaya au jarida ulipendalo," anasema mtaalamu Ryan Peter.

Anasema kwa wanaopenda kukaa chini, wanaweza kuweka mkeka au zulia kulingana na uwezo wa mtu.


Anashauri kuwa kibaraza ni eneo linalohitaji kuwekwa vitu vichache na hasa maua ili liweze kuleta utulivu.

"Unaweza kuweka stand ya kubeba makopo matatu au manne ya maua na kama ni eneo kubwa lenye kona, unaweza kuweka stand mbili za aina hiyo. Maua yawe yanayochanua meupe au pinki ili upate utulivu. Ukiweka yanayochanua rangi nyingi hutokifurahia sana," anafafanua.

Kwa nyakati za jioni, anashauri kuwasha mishumaa miwili au isiyozidi mitano, ili kuweka mwanga.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
HUU MZIGO SIJUI KWA NINI HAUBEBEKI JAPOKUWA NI RAHISI SANA KUJITWISHA!?
JUKWAANI
MSIDHANI NAFAIDI' POSHO NNAZOZIPATA MIMI ZINANIFANYA IBILIZI ANIPANDE KICHWANI ETI NAPANDA NDEGE NAENDA KUOGA ULAYA WAKATI HAPA MIMAJI YA DA'WOSKO IPO TELE INAMWAIKA!
NATAKA KUPUNGUA SILI TENA MBUZI 'NITAKUWA NAPIGA KITIMOTO TU!' NA TUBIA TUWILI DEILE
INABIDI PIA TUTOE TAHADHALI SIKU YOYOTE WAKISIKIA 'PUUU!' WAJUE SIO BOMU
AHADI
UMENIKUTA NA GUMEGUME LANGU UKADHANI NAFAIDI 'ONA UNAVYONYONYOKA KAMA KUKU WA PASAKA!'
SAWA NGURUWE WA KRISMASI LAKINI NITABAKI KUWA BI'MDOGO UPO?
JAMANI KWELI KABISA MMESHUKA KWENYE DALADALA KUMALIZA UBISHI WA NANI KIDUME?
KALETA DHARAU HAWEZI KUNI-KANYAGIA MOKASINI YANGU NAMWAMBIA ANANIVIMBIA!
KIBAYA ZAIDI AMENIITA MWANAMKE INAMAANA HII SURUALI NI SKETI?
BABA SHIDA UKIBOMOLEWA DOMO UJUE UONGOZANI NA MIMI
MWANAUME ANAVUMILIA MANENO MAKALI ISITOSHE UMENI-SUTA WAZIWAZI NIKUITEJE?
UNATAKIWA UELEWE KUWA SIO KILA KITU ANACHOSEMA MWANASIHASA NI KWELI JIONGEZE MAMA...
KWA KUWA ULINIITA PALE JUKWAANI NA KUNINADI KUWA UTANIOA, NIPATIE HIYO MAHALI NISEPE
HAYA NI MAMBO YA KISIASA KWANI KUFAGIA SIKU MOJA BARABARANI NDIO ITAKUWA KAZI YANGU!
SHETANI HAYUKO MBALI 'AUTOMATIKALI' UTAJIKUTA FAGIO LIMEKUNASIA! ALAFU LIMEKUPENDEZA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
....RAHA YA KUFUMANIWA MUULIZE ALIYEFUMANIWA..

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaiwekea Russia vikwazo 500

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imetangaza vikwazo 500 dhidi ya Russia kama mwendelezo wa kuiadhibu nchi hiyo baada ya kuivamia Ukraine na kutokana na kifo cha kiongozi wa upindani Alexei Navalny.

Vikwazo hivyo vipya vinalenga zaidi ya watu 500 na mashirika kutoka nchi tofauti.

Rais wa Marekani Joe Biden, alisema kiongozi wa Russia Vladimir Putin lazima alipe gharama kutokana na uchokozi wake.

"Vladimir Putin lazima alipe gharama kubwa kwa uchokozi wake dhidi ya Ukraine,@ aliandika Rais Biden katika ukurasa wake wa X. Hatua hiyo kali imekuja wiki moja baada ya kifo cha Alexei Navalny na mkesha wa mwaka wa pili tangu kuanza kwa vita nchini Ukraine.

Taarifa kwa vyombo vya habari ya Ikulu ya Marekani ya White House, ilichapishwa seti ya vikwazo vilivyochukuliwa hadi sasa na nchi dhidi ya Russia.

Kwa jumla, vikwazo vipya 500 vinalenga makampuni kutoka nchi 26, watu kutoka nchi 11, ikiwa ni pamoja na China au Ujerumani, pia vinahusu sekta ya fedha ya Russia, sekta ya ulinzi na watu mbalimbali wanaounga mkono Russia.

Aidha, vikwazo hivyo viliwahusisha watu wanaliohusika na kifungo Navalny, ambaye alifariki wiki moja iliyopita akiwa gerezani.

Tangazo hilo la vikwazo vipya pia linakuja siku moja baada ya kufanyika kwa mkutano kati ya Rais Joe Biden na mke na binti wa Alexei Navalny. Maofisa watatu wa Russia ni miongoni mwa wale waliolengwa kwa kuhusika kwao katika kifo hicho, Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ilibainisha, Orodha hiyo inafikisha idadi ya vyombo 4,000 vilivyolengwa na vikwazo vya Marekani tangu kuanza kwa vita.

**RFI**



Wakimbizi wa Sudan wakiwasili nchini Sudan Kusini baada ya kukimbia mapigano yanayoendelea. **PICHA: AFP**

# Mawakili waomba rais aliyepinduliwa kuwa huru

**NIAMEY,** NIGER

MAWAKILI rais wa Niger aliyepinduliwa na wanajeshi, Mohamed Bazoum, wameiomba Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi, ECOWAS, kushinikiza mteja wao aweze kuachiliwa huru.

Katika maombi hayo yaliyowasilishwa katika kikao cha wakuu wa jumuiya hiyo, walisema hatua hiyo ni utekelezaji wa uamuzi wa mahakama.

Mnamo Desemba 15, Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS) iliagiza kuachiliwa kwa rais Bazoum na kurejea madarakani.

"Ni jukumu la ECOWAS na nchi wanachama kuhakikisha kwamba maamuzi ya mahakama yanatumika ipasavyo na kwamba rais Bazoum na mkewe wanaachiliwa huru," alisema Mohamed Seydou Diagne, mratibu wa jumuiya ya wanasheria, katika taarifa kwa vyombo vya habari iliyopelekwa kwa shirika la habari la AFP.

"Mahakama iliagiza mamlaka ya kijeshi kuwaachilia mara moja na kurejesha mamlaka ya rais Bazoum, ambaye mamlaka yake ilikabidhiwa kwake kidemokrasia," walibainisha kundi la wanasheria hao.

Kulingana na mawakili hao, Bazoum hajawahi kufikishwa mahakamani na hajapata kutembelewa na ndugu mbali na daktari wake tangu Oktoba 19, 2023.

Mwanzoni mwa Januari, mtoto wa Bazoum, Salem, aliachiliwa na kuhamishwa mara moja kwenda Togo ambako anaishi kwa sasa.

Hata hivyo, bado anatuhumiwa kwa kula njama zinazolenga kudhoofisha mamlaka au usalama wa Serikali.

Mnamo tarehe 13 Februari, mkuu wa utawala wa kijeshi wa Niger Abdourahamane Tiani, katika mahojiano kwenye televisheni ya taifa alisema kwamba kuachiliwa kwa Bazoum hakuwa kwenye ajenda.

## Marekani yapinga ujenzi nyumba za walowezi

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imelaani pendekezo la nchi ya Israel la kujenga zaidi ya nyumba mpya 3,300 za walowezi wa kiyahudi kwenye eneo la Ukingo wa Magharibi.

Hatua ya kujenga nyumba hizo ni kujibu shambulizi lililofanywa na Wapalestina dhidi ya wayahudi lililotokea wiki hii.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken alisema katika mkutano na waandishi wa habari mjini Buenos Aires, nchini Argentina, kwamba amesikitishwa na tangazo hilo la Israel na kuongeza kuwa makazi hayo yanakiuka sheria za kimataifa na kamwe hayataimarisha usalama wa Israel.

Waziri wa Fedha wa Israel Bezalel Smotrich, alitangaza juzi mipango ya nchi yake kujenga nyumba hizo baada ya Wapalestina watatu wenye silaha kuyafyatulia risasi magari karibu na makazi ya Maale Adumim, na kumuua raia mmoja wa Israel na kuwajeruhi watano.

Takwimu za Umoja wa Mataifa zimeonyesha ongezeko la ghasia za walowezi wa kiyahudi katika Ukingo wa Magharibi tangu kuzuka kwa vita vya Israel na Hamas Oktoba 7, mwaka uliopita.

## Vita Ukraine vyatimiza miaka miwili

**KYIV,** UKRAINE

VITA vinavyoendelea kati ya Russia na Ukraine jana vimetimiza miaka miwili na hakuna dalili ya kumalizika mapema.

Uvamizi huo uliotekelezwa na Russia umesababisha nchi hiyo kuingia katika mgogoro na Marekani na mataifa ya Ulaya tangu kumalizika kwa vita vya pili vya dunia. Wachambuzi wa masuala ya kimataifa walisema kuwa mwaka huu utashuhudia makabiliano makali, wakati Ukraine ikitarajia kuchukua maeneo yake yanayokaliwa na Russia.

Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, kupitia mtandao wake wa X, alieleza kuwa nchi yake haitachoka kuiunga mkono Ukraine katika vita vyake na Russia.

Hata hivyo, Ukraine imeapa kupata ushindi dhidi ya Russia katika kuitetea ardhi yake wakati vita hivyo vikiingia katika mwaka wake wa pili.

Jitihada za nchi hiyo kufanya mashambulio zimeonekana kupungua kutokana na ukosefu wa usambazaji wa silaha inazohitaji kutoka kwa washirika wake nchi za Magharibi.

Wakuu wa nchi za G7 wanatarajiwa kukutana kwa njia ya mtandaoni kuadhimisha miaka miwili ya vita hivyo, huku Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky akiwa miongoni mwa watakaohudhuria.

Waziri mkuu wa Italia Giorgia Meloni, ambaye ni mshirika wa Ukraine aliwasili nchini Ukraine kwa ajili ya maadhimisho ya miaka mwili ya vita, akitarajiwa kuongoza kikao cha mtandao cha viongozi wakuu wa G7.

**RFI**

MAKALA

# WARAKA KWA WAZIRI WA ELIMU



Na Magabilo Masambu

**Kimsingi, elimu ndiyo ufunguo wa maisha lakini kuna wakati inaweza kuwa kufuri la maisha. Ukijaribu kutazama maeneo mengi hasa vijijiji, bado kuna changamoto za kimazingira za kujifunzia na kufundishia. Walimu katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji watazamwe kwa namna ya pekee.**

NI ukweli kwamba nchi yetu ni kubwa na pengine inaweza kuonekana kuwa rasilimali tulizo nazo hazitoshelezi kuboresha maisha ya watu kwa kiwango ambacho kila mtu ataridhika. Lakini waswahili wanasema kupanga ni kuchagua, hivyo kama nchi lazima tuwe na vipaumbele. Inawezekana mambo yote yakawa muhimu lakini kuna ya muhimu zaidi.

Elimu katika taifa lolote lazima kiwe kipaumbele cha kwanza kabisa kwa sababu mambo mengine yote hutokana na elimu. Hatuwezi kuwa na taifa imara kama mfumo wa elimu si imara.

Mfumo wa elimu pekee pia hautoshi, lazima tuwe na watu walio tayari kuutekeleza na katika kutekeleza, lazima kuwe na mazingira mazuri ya utekelezaji.

Mtekelezaji wa kwanza wa mfumo wa elimu ni mwalimu ambaye amepewa mamlaka kisheria katika utekelezaji wa mtaala wa elimu. Serikali inasimamia utekelezaji huo na wanafumzi ni wapokeaji wa maarifa yaliyomo katika mtaala huo.

Kwa hiyo, serikali pamoja na kwamba inayo mamlaka ya kuhakikisha mtaala unatekelezwa, pia inao wajibu wa kuhakikisha mazingira ya ufanyaji kazi wa watumishi katika sekta nzima ya elimu yanaboreshwa na kuwa rafiki.

Ni kweli kwamba juhudi mbalimbali zimefanyika lakini bado yanahitajika mapinduzi makubwa katika kuhakikisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yanakuwa mazuri zaidi kwa walimu na wanafunzi ili elimu itokanayo na utekelezaji huo, iwe na tija kwa wahitimu wenyewe na kwa taifa pia.

Kimsingi, elimu ndiyo ufunguo wa maisha lakini kuna wakati inaweza kuwa kufuri la maisha. Ukijaribu kutazama maeneo mengi hasa vijijiji, bado kuna changamoto za kimazingira za kujifunzia na kufundishia.

Walimu katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji watazamwe kwa namna ya pekee.

Pengine wizara yenye dhamana ya elimu na serikali kwa ujumla, watenge fedha za kuwalipa walimu malipo ya mazingira magumu zaidi ya mishahara yao wanayoipata kila mwezi.

Kuna wakati walimu hawa wanasafiri umbali mrefu kufuata huduma za kiofisi kwa kutumia gharama kubwa kama nauli ambazo zinatoka kwenye mshahara ule ule na kufanya maisha yao kuwa duni, jambo linalowafanya washindwe kupiga hatua za maendeleo binafsi.

Kuna uhusiano wa karibu kati ya utulivu wa nafsi na utendaji kazi mzuri na wenye tija. Kama walimu hao watakuwa wanawaza zaidi namna gani watajikwamua katika mazingira magumu, inaathiri pakubwa katika utendaji wao wa kazi, hivyo mwisho wa siku wanafunzi wanashindwa kupata kinachowastahili.

Asilimia kubwa ya walimu walioajiriwa maeneo ya vijijini wanatumia muda wao mwingi kufikiria namna ya kuhama huko.

Lakini jambo linaloumiza zaidi ni kuhusu kuhama huko kwamba mwalimu akitaka kuhama anaambiwa atafute wa kubadilishana naye. Wakati mwingime anampata lakini bado vikwazo vinajitokeza.

Tunawatwisha mizigo mikubwa walimu hawa, hivyo lazima kufanyike jambo ili kuwafanya wanapokuwa huko vijijini wasiwaze kuhama badala yake wawatumikie watanzania wenzetu walioko huko.

Ndugu Waziri, ni kweli kwamba miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ni muhimu sana ndiyo maana serikali inaweka nguvu kubwa katika kujenga madarasa ili kukabiliana na wingi wa vijana wetu wanaoongezeka kila mwaka.

Ni muhimu sasa ujenzi huu wa madarasa uendane na ujenzi wa nyumba za walimu kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan amewahi kuahidi ili kuondoa adha ya walimu kudaiwa kodi za pango.

Kuna mazingira mwalimu anaweza kupangiwa kituo na hakuna hata nyumba za kupanga zaidi ya nyumba chache za wenyeji, jambo linalomlazimisha mwalimu kupanga mbali na eneo lake la kazi.

Inawezekana hatupati elimu ya pamoja au watoto wetu si walimu, kwa hiyo kuziona changamoto hizi inakuwa ngumu. Wakati fulani tutoke ofisini tuwatembelee huko vijijini ndipo tutaona hali ilivyo. Pamoja na hayo yote, ni muhimu kuelewa kwamba walimu wengi wanapitia changamoto nyingi hasa hawa walio pembezoni mwa miji kiasi cha kuwafanya wengine wawe na msongo wa mawazo na kutumia muda mrefu kuwaza namna gani watatoka huko badala ya kutumia muda mwingi kuwaandaa na kuwanoa vijana wetu.

Huko pembezoni pia kuna Watanzania wanaohitaji huduma ya elimu, hivyo tusingependa kuona walimu wanahama na kuwakimbia Watanzania wenzetu.

Jambo la muhimu ni serikali kupitia wizara yako kuboresha mazingira na masilahi ya walimu hao ili Watanzania hao waendelee kuelimika.

Kama wakuu wa shule na waratibu kata wanapata posho za madaraka, vipi kuhusu walimu wanaopambana na watoto wetu darasani na nje ya darasa? Nafikiri ni jambo linawezekana na ikishakuwa hivyo, hutaona mwalimu anaomba kutoka huko vijijini na kung'ang'ana kurudi mjini.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kisa jamaa aliyeoa mke wa mtu aliyefungwa jela*



Na Adam Fungamwango

**Miaka ikazidi kusonga mbele, mara tabia ya mwanamke ikaanza kubadika. Akaanza kuwa na kidomodomo, kususa, maneno mengi, kashfa, dharau, kejeli, ili mradi tu nyumba tena haikuwa na amani.**

DUNIANI kuna mitihani sana. Wewe fikiria, unapata mwenza, unafunga naye ndoa, kumbe mwenzako alishafunga ndoa siku nyingi lakini hayuko naye kwa sasa kwa sababu ya matatizo mbalimbali.

Hajaachana naye wala nini. Ni mazingira tu ndiyo yamewaachanisha. Kama mwanamume anakuoa ili asogeze siku hadi matatizo ya mkewe yamalizike. Na kama mwanamke anamsubiri mumewe siku atakaporudi.

Kisa hiki kinasimuliwa kwenye wimbo wa Juwata Jazz, wana Msondo Ngoma, ambacho kinazungumzia jamaa aliyekutana na mwanadada mrembo, akampenda, amamwuliza kama hana mume akajibiwa naaam.

Mwanamume akajitosa, akamuoa. Kumbe ilikuwa ndoa ya pili na batili. Mwanamke huyo alikuwa ameshaolewa na mwanamume mwingine. Hayuko naye kwa sasa kwani amefungwa jela miaka mingi na asingeweza kutoka hivi karibuni.

Mwanamke akapiga hesabu miaka kibao ambayo mumewe halisi yuko gerezani asingeweza kujihudumia kwa mavazi, chakula, vipodozi, kajifanya yuko singo. Ndoa ikafungwa, mume na mke wakaishi raha mustarehe na Mungu akawajalia wakapata mtoto wa kiume.

Miaka ikazidi kusonga mbele, mara tabia ya mwanamke ikaanza kubadika. Akaanza kuwa na kidomodomo, kususa, maneno mengi, kashfa, dharau, kejeli, ili mradi tu nyumba tena haikuwa na amani.

Mume akaona kabda kuna kidudu mtu anasababisha wagombane. Akaanza kuchunguza lakini wapi.

Siku isiyo na jina, aliporudi kazini hakumkuta mkewe nyumbani. Akauliza majirani wakamjibu hawajui alikokweda na mtoto kamwacha. Baada ya siku kadhaa kuna mtu akamwambia alimwona mama watoto wake mitaa ya Kariakoo, akipanda basi la kwenda Mbeya.

Ikumbukwe kuwa zamani miaka ya 1980, wakati wimbo huo unarekodiwa, abiria walikuwa wakipanda baasi ya mikoani mitaa ya Kariakoo na Kisutu jijini Dar es Salaam. Hakuna kinachofikika katika sayari hii ya dunia kikakosa kujulikana. Uongo unaweza kufichwa kwa miaka karne moja, lakini iko siku tu ukweli utabainika.

Ikaja kubainika kumbe jamaa alioa mwanamke ambaye alikuwa mke wa mtu.

Alidanganywa kuwa hajaolewa, kumbe haikuwa hivyo kwani mumewe halisi alikuwa amefungwa jela miaka mingi na ingechukua kuda mrefu kutoka ndiyo maana akaamua kuolewa.

Waswahili wanasema siku hazigandi, miaka ilipokuwa ikikaribia, dada alijua kabisa kuwa miaka ya mumewe kurudi inakaribia. Kwa maana hiyo alichofanya ni kitengeneza mazingira ya kuiua ndoa batili ili arudi kumpokea mumewe halisi aliyekuwa anatarajia kumalizza kifungo.

Siku ilipowadia akamtoroka mume batili, akarudi Mbeya ambako alikuwa anaishi na mumewe halisi.

Wimbo huu ulitungwa na aliyekuwa kiongozi wa bendi hiyo, Said Mabera, ukaimbwa na kina Fresh Jumbe, Hamisi Kitambi, Juma Akida na Joseph Lusungu.

Unaeleza kuhusu baadhi ya mambo ambayo huwezi kufikiria kuwa yanafanyika ndani ya jamii yetu.

Lakini humu ndani ya jamii kuna mambo mengi na ya kushangaza ambayo baadhi yao wamehadithiwa kwenye nyimbo hasa za zamani.

Haya ndiyo mashairi halisi ya wimbo huo uliopewa jina la 'Kenjelenjele' ambalo ndiyo jina la mwanamke aliyefanya kituko hicho.

"Nilitegemea nitaishi naye, kumbe haikuwa hivyo, alinieleza kama hana mume nikaamua kuwa naye, alinieleza kama hana mume nikaamua kuwa naye, muda tulioshi pamoja tulijaliwa kupata mtoto, siku zote nilikuwa sielewi, kumbe mume wake alikuwa jela. Alipoona muda umekaribia aaa, wa mumewe kutoka kifungoni ee, alianza visa na kashfa nyingi, baadaye mama akanitoroka."

"Kanjelenjele mama, Kanjelenjele mama, sikutegemea kama ataningeuka Kanjele."

"Nilipotoka subuhi na mapema, niliporudi nyumbani, sikumkuta Kanjele nyumbani.

Rafiki na jirani zangu walinielezea, walimuona Kariakoo, akipanda basi kwenda kwao."

Ulipokuwa ukipigwa kwenye kumbe za dansi, kipande cha alichoimba Lusungu alikuwa anaimba hivi: "Rafiki na jirani zangu walinielezea, walimuona Kariakoo, akipanda basi kwenda Mbeya."

Lakini walipoingia studio za Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) wakati huo, wakaambiwa watoe neno Mbeya na ilifanyika hivyo ili isionekana kama watu wa huko ndio wana tabia hiyo.

Kwa busara tu za kamati ya kupitisha, wakaona bora liwekwe neno ambalo halitautaja mkoa wowote, ndipo walipokubaliana kuwa waweke neno 'kwao' ambalo halitojinasibisha na mkoa au eneo lolote. Hivyo ndivyo vituko kwa mwanamama Kanjelenjelena kisa cha jamaa kuoa mke wa mtu ambaye mumewe alikuwa jela.

**Tuma meseji 0716 350534**

HADITHI

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi Kichefuchefu - 12

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"VIPI mke wangu, mbona hivi?" Akauliza.

"Ndiyo vivyo unavyoona. Naondoka!"

"Unaondoka? Kwani kumetokea nini?"

"Unasikia mume wangu, bora mimi niondoke kuliko siku ukirudi ukute maiti hapa!"

"Kwani kumetokea nini?"

"Kama siyo majirani basi leo ungekuta maiti moja, au mbili yangu na dada yako! Au basi kama siyo hivyo, mmoja yupo hospitali, mwingine polisi, au wote wawili hospitali!"

"Mmepigana?"

"Nasema hivi, alitaka kunipiga, nimemkwepa, akajigonga kwenye mlango wetu huu. Ana bahati nilitaka nimmalize hapa hapa dada yako. Haiwezekani anitukane mimi na ukoo wangu, yaani sisi kwetu masikini! Ukweli imeniuma sana na kwa hiyo ninachokwambia, naenda kwa dada yangu, nalala kesho asubuhi kwetu, Kondoa."

"Unaenda Kondoa!?" Kassim akashangaa na kushtuka kwa wakati mmoja.

"Sasa kwetu wapi? Ulipokuja kukunja goti na kunioa ni wapi? Akaulizwa na mkewe.

Wakati akikuna kichwa nini afanye, sauti ya mkewe ikarindima tena masikioni mwake.

"Sasa ndiyo utaamua, nani akae hapa, mimi au dada yako. Nakwenda kwetu, nitarudi pale nitakapohakikisha kuwa dada yako hayupo tena hapa."

Ukweli ni kwamba Sauda hakutaka kuondoka. Ulikuwa ni mpango tu ambao ameutengeneza mwenyewe ili kumpa shinikizo mumewe.

Alijua akifanya hivyo mumewe atapagawa na kuchukua hatua. Ni kwa sababu anampenda.

Sauti za shoga yake Paulina na shoga wa wifi yake Fatuma walishamwambia apiganie ndoa yake.

Asiikimbie kwa sababu ya wifi yake. Sasa alikuwa ameshapanga plani yake.

Alijua sasa mumewe, ama yeyote yule mwenye mapenzi mema na yeye anaweza akaamua hili vizuri ili aishi vyema katika ndoa.

Kassim kwa jinsi alivyoona tu alikuwa mkewe yupo njia moja kuondoka. Alivyomkuta na mabegi yake aliona kabisa kuwa atamkosa mke.

Na yeye pia aliwahi kuambiwa na rafiki ya mkewe asuke au anyoe, la sivyo atamkosa mke.

"Wewe mwanaume ukilemaa nakwambia mke huna. Ipo siku ataondoka na kukuacha na dada yako mbaki mnatumbuliana macho. Havijawa ni shoga yangu, lakini kwa alichomfanyia yule dada sijakipenda.

Lazima uongee na dada yako, au ufanye kitu ambacho kitamaliza hili tatizo, vinginevyo jiandae kumkosa mke.

Mimi siwezi kukupa ushauri wa kumkandamiza mkeo, au dada yako. Uamuzi unao mwenyewe kaka kusuka au kunyoa."

Maneno aliyoambiwa na Fatuma, shoga ya dada yake yalijirudia tena kichwani mwake.

Alichofanya alitoka kwenda kwa dada yake. Alipofika mlangoni kwake aligonga hodi.

Havijawa alikuwepo, akatoka nje. Wote wawili walivyoangaliana ilionekana kabisa kuna jambo.

Kassim alikuwa na hasira kwa jinsi alivyoambiwa na mkewe. Havijawa alijua kuwa ameitwa kwa ajili ya ule ugomvi na si kitu kingine.

"Havijawa! Hivi wewe na wifi yako kila siku mnagombania nini? Mbona mnatia aibu? Na wewe ndiyo mgomvi, maambiwa na watu wengi, majirani, na watu wengine wa heshima zao kuwa unamsemasema, unamnyanyasa mke wangu.

Kwa nini hutaki kuona akiishi hapa kwa furaha?"

"Umemaliza?" Havijawa akauliza kwa nyodo akiwa ameweka mikono kiunoni, akimtazama kaka yake kuanzia chini hadi kichwani.

"Sijamaliza!" Akajibu kwa sauti ya juu na ya hasira. "Sikiliza, kama wewe umeshindwa kuishi na mwanaume wako kule Keko, usitake kuivunja ndoa yangu.

"Kaka usitake nikuvunjie heshima. Kuoa isiwe sababu ya kuvunja undugu wetu, mimi na wewe ni mtu na dada yake, lakini leo naona unaniita jina langu tu, Havijawa, dada tena limekufa?" alisema kwa sauti ya dhihaka.

"Halafu sikiliza nikwambie, hao watu sijui majirani wanaokwambia mimi namnyanyasa mkeo, mbona hawaji kukwambia kuwa mkeo anatembea na mwanaume mmoja nyumba ya jirani.

Wanaliona hilo tu." Havijawa akaongopa ili kupoza joto la kaka yake, lakini pia kuona kama anaweza kuugeuza ugomvi ukawa baina ya mume na mke, badala ya kaka na dada.

"Mimi nakuulizwa suala lingine, kwa nini ulikuwa unataka kumpiga mke wangu?"

"Hivi wewe mzima kweli, au umeshatiliwa limbwata na mkeo. Yaani mkeo anitukane mimi nimtazame tu."

"Lini mke wangu ameanza kutukama, namfahamu, hajawahi kuwa na tabia hiyo, wewe nakufahamu una ya aina hiyo. Wewe ni mgomvi dada yangu. Yaani mke wangu hana furaha kabisa."

"Kwa hiyo ulikuwa unataka mimi ndiyo nimpe furaha? Umesharogwa wewe kaka yangu si bure. Hivi unajua mkeo kanitukana kiasi gani mimi?"

Havijawa alizidi kucharuka.

"Amesemaje?"

"Yaani mimi sijafundwa, shangazi yangu hajafundwa, marehemu mama hajafundwa, katukana mbele za watu wote wanasikia." Havijawa alizidi kuongopa ili Kassim amuone mkewe ndiyo muongo na mwenye makosa. Aliposema hayo akaanza kuangua kilio.

> **"Yaani mimi sijafundwa, shangazi yangu hajafundwa, marehemu mama hajafundwa, katukana mbele za watu wote wanasikia." Havijawa alizidi kuongopa ili Kassim amuone mkewe ndiyo muongo na mwenye makosa. Aliposema hayo akaanza kuangua kilio.**




Uongo na uigizaji wa Havijawa ulimtoa kwenye reli Kassim. Ile presha aliyokuja nayo ilipungua na sasa alianza kujiona kama hakufanya vyema kwenda kumuuliza dada yake.

Hajasahau pia kuwa mkewe yupo chumbani na mabegi, akisubiri tu atakayoambiwa na mumewe baada ya kurudi kwa dada yake.

Kassim alichezewa mchezo na watu wawili, dada na mkewe. Mkewe alijifanya anaondoka akapanga mabegi yake. Dada yake anaangua kilio akidai wifi yake amemtukana matusi ya nguoni yeye na baadhi ya watu wa ukoo wao.

"Kwa nini unalia sasa? Haya si tunayazungumza tu?"

"Nawakumbuka marehemu baba na mama, wamekufa wametuacha mimi na wewe. Wewe ndiyo nakutegemea, lakini naonekana takataka mbele ya mwanamke ambaye amekuja tu, sijui hata ametokea wapi. Amekuja kutufarakanisa mimi na kaka yangu." Havijawa alizidi kutengeneza maigizo.

Kassim alipoona kilio kinazidi akaamua kuondoka kurudi chumbani kwake ambako amemuacha mkewe.

Alipoohakikisha kuwa kaka yake ameondoka akanyamaza, akatabasamu na akacheka kicheko cha kebehi.

"Kwenye misiba tu silii nilie kwa ajili hii. Hee! Nitahakikisha anatoka mbwa yule, huu ni mwanzo tu, mwanamke amekuwa kero, kuzaa hazai, kupika hajui, usafi matatizo, hata kujisafisha mwenyewe hawezi, atatoka, mimi siyo Havijawa.

Alipoingia ndani na yeye akatengeneza igizo kwa mkewe. "Nimempa vipande vyake huko hadi analia."

Mkewe aliposikia hivyo presha ikamshuka, akaanza kuvua nguo zake za safari na kurudisha mabego yake yalipokuwa awali.


"Ukweli mume wangu kwa hili, ni lazima kitu kifanyike. Haiwezekani na hitowezekana tukaendelea kukaa hivi."

"Ni kweli, nimekuwa napata ushauri kutoka kwa watu mbalimbali kuhusu hili, siku chache zijazo nataka kuchukua maamuzi magumu.

**INAENDELEA JUMAPILI**

## HABARI BURUDANI

# RICK ROSS KUITANGAZA AFRIKA



Rapa wa Marekani Rick Ross ameazimia kutangaza utamaduni wa Afrika kwa kufanya kolabo na baadhi ya wasanii wa Afrika, akianza na Nigeria.

Katika vedeo yake iliyoitoa juzi, msanii huyo wa hip hop alisema anataka kuonyesha upendo kwa viongozi na marais wa Afrika, zikiwemo nchi za Ghana na Nigeria, huku akianza na Rais Bola Tinubu.

"Nataka kuonyesha upendo kwa marais wa baadhi ya nchi hizi za ajabu. Ninatakatu kuleta utamaduni na wasanii wa ajabu, wacha tuanze na Nigeria kwa Rais Tinubu!" Alisema rapa huyo, Mmarekani mwenye asili ya Afrika.

Maneno yake hayo yanashabihiana na dhamira yake ambapo hivi majuzi alifichua nia yake ya kutaka kufanya kolabo na baadhi ya wasanii wa Afrika, wakiwemo Asake, Odumodublvck, Stonebwoy, Black Sheriff wa Ghana, na Nasty C kutoka Afrika Kusini kwa ajili ya albamu yake ya hivi karibuni, iitwayo, 'Champagne Moments'.

Rapa huyo mwenye umri wa miaka 48 amewahi kufanya kolabo na P-Square, Yemi Alade, na Diamond Platnumz wa Tanzania.

# Pole sana Wendy Williams



MKALI wa kipindi cha mazungumzo nchini Marekani, Wendy Williams Hunter, agunduliwa kuwa na matatizo ya ubongo ya (FTD), imefahamika.

Timu ya madaktari wake imeamua kuweka wazi kwa kile ilichodai, "ili kurekebisha uvumi usio sahihi na wa kuumiza kuhusu afya yake".

Bi Williams, 59, alikuwa mwenyeji wa kipindi cha Wendy Williams Show kilicho na umaarufu mkubwa kilichokwenda hewani nchini Marekani kwa zaidi ya muongo mmoja, hadi kilipomalizika 2022.

Habari za kugunduliwa kwa matatizo hayo zinakuja siku moja baada ya jarida la People Magazine, ambapo jamaa walisema Bi Williams yuko chini ya uangalizi katika eneo lisilojulikana na amekuwa katika hali isiyoridhisha kiafya.

"Kama mashabiki wa Wendy wanavyofahamu, siku za nyuma amekuwa wazi kwa umma kuhusu mapambano yake ya kimatibabu, ugonjwa na changamoto zingine muhimu zinazohusiana na afya yake," timu yake ya madaktari na ya kumtunza iliandika katika taarifa hiyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BRUYNE AWINDWA UARABUNI

MANCHESTER City inajidhatiti kufikiria ombi kutoka kwa Klabu za Saudia kumnunua kiungo wa kati wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 32. Na Itachukua ofa ya zaidi ya pauni milioni 100 kumuuza De Bruyne. (***Talk-sport***)

### SANCHEZ KUUZWA

CHELSEA iko tayari kumuuza mlindalango wa Hispania, Robert Sanchez mwenye umri wa miaka 26, msimu huu na wanaweza kumleta kipa wa Arsenal, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 25 kama mbadala wake. (***HITC***)

### YILDIZ KWENYE RADA

ARSENAL inavutiwa na mshambuliaji wa Juventus, Kenan Yildiz mwenye umri wa miaka 18, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Uturuki pia yuko kwenye rada za Liverpool na Borussia Dortmund. (***Calciomercato***)

### KOUNDE AFUATILIWA CHELSEA

CHELSEA imekuwa ikimfuatilia mlinzi wa Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 25 kutoka Barcelona kwa ajili ya kumsajili msimu ujao. (***Fichajes***)

### BALLARD ATAKIWA EVERTON

KLABU ya Everton inatazamiwa kumlenga beki wa Sunderland, Dan Ballard mwenye umri wa miaka 23, ikiwa Jarrod Branthwaite mwenye umri wa miaka 21, ataondoka Goodison Park msimu wa joto. (***Football Transfers***)

### RODRIGUEZ KUNUNULIWA

KLABU ya Manchester United inaweza kumnunua kiungo wa kati wa Real Betis, Guido Rodriguez mwenye umri wa miaka 29, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina akiwa huru kufanya mazungumzo ya awali ya mkataba mpya na Klabu za Hispania, huku mkataba wake wa sasa ukikamilika msimu wa joto. (***Fichajes***)

### VARANE ATAKIWA SAUDI

KLABU za Saudi za Al-Ittihad na Al-Nassr vinamlenga beki wa Manchester United mwenye umri wa miaka 30, Raphael Varane msimu huu wa joto. (***90 min***)

### UNITED YAMFUATILIA BREMER

KLABU ya Manchester United inamfuatilia beki wa Juventus, Gleison Bremer mwenye umri wa miaka 26 kama mbadala wa Raphael Varane na wanaweza kutoa kati ya euro milioni 60 hadi 70 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil. (***Tuttosport***)

### BRIGHTON YAMTAKA CASEY

BRIGHTON ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazomtazama mshambuliaji wa Charlton Athletic raia wa Ireland, Patrick Casey, mwenye umri wa miaka 18. (***Football Insider***)

### CALHANOGLU AIKATAA SAUDIA

KIUNGO wa kati wa Uturuki, Hakan Calhanoglu mwenye umri wa miaka 30 amesema alikuwa na ofa ya kuhamia Saudi Arabia, lakini anataka kubakia Inter Milan. (***DAZN, kupitia Gazzetta dello Sport***).

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NI CHELSEA VS LIVERPOOL FAINALI CARABAO CUP

**LONDON,** England

Vigogo wa darajani wanalenga kushinda taji lao la kwanza ndani ya miaka sita huku majogoo wa Anfield wakitaka......

CHELSEA itacheza na Liverpool kwenye fainali ya Kombe la Carabao leo Jumapili huku ikilenga kushinda taji lake la kwanza la nyumbani kwa kipindi cha miaka sita, huku Wekundu hao wakiwa kwenye nafasi ya kushinda la kwanza kati ya manne wanayoyawania msimu huu.

Mchezo huo ni wa marudiano wa fainali za Carabao na FA za mwaka 2022, huku Liverpool wakishinda zote kwa mikwaju ya penalti.

Wekundu hao wanaongoza Ligi Kuu kwa pointi nne na wako kwenye hatua ya 16 bora ya Ligi ya Europa na Kombe la FA raundi ya tano. "Tutakubali," alisema kocha msaidizi wa Liverpool, Pep Lijnders.

"Ni mchezo maalum. Michezo maalum inahitaji maonesho maalum kwa hiyo tunapaswa kuzingatia uchezaji."

Huku Lijnders na kocha Jurgen Klopp wakikaribia kuondoka Anfield msimu huu wa joto, mashabiki wa Liverpool wanatamani wafurahie ushindi wakiwa tayari wameshinda mataji sita makubwa tangu Klopp aanze kuinoa timu hiyo mwaka 2015.

"Falsafa yetu ni kutoa furaha na hisia kwa mashabiki," aliongeza Lijnders. "Nina furaha sana kwamba tunaweza kutoa angalau fainali kwa kuanzia."

**Beki Virgil van Dijk, ambaye atakuwa nahodha wa Wekundu hao katika fainali ya Wembley kwa mara ya kwanza kesho, alisema: "Tunataka kuifanya siku maalum na kupata kombe letu la kwanza msimu huu.**

"Mwisho wa msimu pengine utakuwa wa hisia sana kwa watu wengi, akiwemo kocha, lakini bado hatujafika. Hatupaswi kuangalia mbele sana, tunapaswa kuangalia kilicho mbele yetu."

Taji la mwisho la Chelsea la nyumbani lilikuwa Kombe la FA mwaka 2018, ingawa walishinda mataji manne ya kimataifa baada ya hapo, la hivi punde zaidi likiwa Kombe la Klabu bingwa ya dunia waliloshinda mwaka 2022 wiki mbili kabla ya kushindwa na Liverpool kwenye fainali ya Kombe la Carabao mwaka huo.

Kocha Mauricio Pochettino, ambaye alichukua jukumu pale Stamford Bridge msimu uliopita wa joto, anaweza kushinda taji lake la kwanza nchini England baada ya misimu ya awali ya kuinoa Southampton na Tottenham Hotspur.

"Ina maana kubwa kwetu, wafanyakazi na makocha, kufika fainali na kutoa changamoto kwa timu kama Liverpool," alisema raia huyo wa Argentina.

"Ni ndoto kwetu, tunayo nafasi na tunaenda kupambana. Nadhani timu iko tayari na tutakuwa na ushindani mkubwa."

# TUCHEL: SIO MIMI PEKEE MWENYE TATIZO BAYERN



**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel amesema sio yeye pekee aliyehusika na mwenendo mbaya wa timu yake na kuongeza kuwa uamuzi wa klabu hiyo kuachana naye mwishoni mwa msimu utampa "uhuru zaidi".

Bayern wiki hii waliamua kutangaza kuachana na Tuchel mwishoni mwa msimu huu, licha ya mkataba wake kuendelea hadi 2025 baada ya kupoteza mechi tatu katika mashindano yote.

Miamba hao wa Bavaria, ambao wameshinda mataji 11 ya awali ya ligi nchini Ujerumani, wako katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, pointi 11 nyuma ya vinara Bayer Leverkusen.

"Haijalishi kama ninaelewa uamuzi wa klabu au kama ninafurahishwa nao," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari.

"Kitu pekee cha muhimu sasa ni kwamba kuna uwazi. Uwazi huleta uhuru na ni mzuri kwa mechi na mazoezi.

"Uhuru zaidi kwa kocha juu ya jinsi ya kutenda. Hufai kufikiria matokeo ya muda mrefu ya uchaguzi wako," alisema. "Unaweza kuwa mzembe zaidi."

Tuchel alikuwa amechukua nafasi hiyo Machi 2023 kutoka kwa Julian Nagelsmann huku akiwa na matarajio makubwa, lakini alianza vibaya na kuambulia patupu kwenye Kombe la Ujerumani na Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya kunyakua taji la Bundesliga kutoka kwa Borussia Dortmund siku ya mwisho ya msimu.

Msimu huu wamekuwa hawatabiriki, wakionesha mwanga mdogo tu wa namna ambavyo imewafanya kutawala soka la Ujerumani kwa zaidi ya muongo mmoja.

Waliondolewa katika Kombe la Ujerumani la mwaka huu na klabu ya daraja la tatu Saarbruecken, pia waalipoteza mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa baada ya kufungwa 1-0 na Lazio ya Italia.

"Sifikirii kuwa mimi pekee ndiye tatizo, lakini nakubali wajibu wangu. Sijaridhishwa na jinsi tunavyocheza na nimekuwa sina furaha kwa muda mrefu."

"Sasa tuna hali mpya, lakini hali hiyo imetatuliwa na kuwasiliana lakini sidhani kama mimi pekee ndiye tatizo."

# Wenger aionya Liverpool kuhusu kocha

**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger amewaonya mabosi wa Liverpool kwamba wasimtumie Jurgen Klopp kama mshauri wa kupendekeza Kocha mpya atakayechukuwa mikoba yake baada ya yeye kuondoka mwisho wa msimu.



Klopp ambaye ataondoka Liverpool mwisho wa msimu huu ikiwa ni baada ya kuhudumu kwa miaka tisa, hivi karibuni alifanya mahojiano na kusema kwamba Xabi Alonso ni mmoja kati ya makocha wanaofaa kuifundisha timu hiyo.

Kocha huyu amekuwa sehemu ya mabadiliko ya Liverpool akihusika kwenye masuala mbali mbali kuanzia akademi na usajili na amekuwa mshauri mkubwa wa mabosi wa timu hiyo.

Lakini Wenger ambaye alidumu kwenye kikosi cha Arsenal kwa zaidi ya miaka 20, amesema kama wamiliki wa Liverpool watasikiliza ushauri wa Klopp juu ya kocha mpya hilo litakuwa ni kosa kubwa wamelifanya.

"Hapana hapana. Sifikirii kama hilo linafaa labda wawe wamemuajiri rasmi kama mshauri wa timu, inatakiwa ufanye kazi yako na uache watu wengine wafanye kazi yao, nafikiri timu inafanya kazi vizuri pale kila mtu anapofanya majukumu yake, mwisho wa siku wewe kama mmliki unakuwa unajua kama mambo hayajaenda sawa nani inabidi umuulize." amesema Wenger alipofanya mahojiano na BeIN Sport na aliweka wazi jinsi yeye alivyowaacha Arsenal wafanye kazi yao ya kutafuta kocha mpya baada yeye kuondoka mwaka 2018 ambapo yeye hakuhusika kabisa.

Hata hivyo, Klopp mwenyewe amewahi kusema kwamba hatahusika kabisa kwenye masuala ya kupendekeza Kocha mpya.

"Hapana, kwa nini nifanye hivyo, inaonekana kama nafanya kazi zote, lakini sio kweli na siwezi kufanya hivyo, mambo yote yaliyotokea kwa zaidi ya miaka minane nikiwa hapa ni kwa kushirikiana." amesema Klopp

# Varane sasa ageuka lulu Saudia

**MANCHESTER,** England

MLINZI wa Manchester United, Raphael Varane ndiye anayelengwa zaidi nchini Saudi Arabia katika uhamisho wa majira haya ya joto huku Al Ittihad na Al Nassr zikishughulikia kutoa ofa kwa sasa, kwa mujibu wa 90min.

Mkataba wa Varane kule United unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2023/24, ingawa klabu hiyo haijakataa kuongezwa kwa masharti yaliyopunguzwa, sawa na majaribio ya mwisho ya msimu wa joto ambayo hayakufaulu kumbakisha David de Gea.

Beki huyo ana matumaini ya kuepuka hali kama hii, ambapo haikufahamika iwapo kipa huyo wa Hispania angepokea ofa ya mkataba mpya baada ya mkataba wake wa awali kumalizika.

Maslahi ya Varane yataongezeka kule Saudia, kwani Al Ittihad inatayarisha ofa yenye thamani ya karibu euro milioni 30 kwa msimu, na fursa zingine za mapato zaidi.


Tayari wameshawasiliana kwa maneno na kambi ya Varane kuelezea ofa yao.

Al Shabab pia wamemjadili Varane, lakini itakuwa vigumu kwa klabu isiyodhibitiwa na PIF kuingia kwenye kinyang'anyiro hicho.

PIF wana hisa za kuidhibiti Al Ittihad, Al Nassr, Al Ahli na Al Hilal.

Al Ittihad na Al Nassr wanatumaini kumpata Varane kwa mkataba wa miaka mitatu iwapo wataendelea na majaribio ya kumsajili.

Kama ilivyo kwa N'Golo Kante kwenda Al Ittihad, wafanyabiashara wa kati huenda wakaamua klabu ya mwisho ambayo atatua.



## Mashindano kuogelea yashika kasi Dar

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya kuogelea ya vijana ya Taliss yanaendelea tena leo huku vijana wakionyesha upinzani mkubwa na kuonyesha vipaji vyao kwenye mchezo huo.

Mashindano hayo yaliyoanza jana yanafikia mwisho leo kwenye bwawa la kuogelea la shule ya kimataifa ya Tanganyika (IST).

Akizungumza jana baada ya funguzi wake, Mratibu wa mashindano hayo, Alexander Mwaipasi alisema mashindano hayo yamekuwa na ushindani mkubwa kwani waogeleaji wengi wameonyesha uwezo mkubwa na wengine kuvunja rekodi zao za muda.

Aidha, alisema mashindano ya mwaka huu wamejitahidi kuboresha kwa kiasi kikubwa zawadi kwa washindi pamoja na uwendeshwaji wake. "Lengo la mashindano hayo ni kuangalia vipaji vya watoto, kwa sasa mchezo huu umezidi kushika kasi tofauti na miaka iliyopita kwani watu wengi wameanza kuufahamu na kushiriki kucheza au kuleta vijana wao kushiriki," alisema Mwaipasi na kuongeza,

"Tangu mashindano yaanze wachezaji wengi wameweza kuvunja rekodi kwani wameonyesha uwezo mkubwa jambo linalotupa matumaini kuona vipaji vinazidi kukua," alisema.

Alisema mashindano hayo ya mwaka huu yameshirikisha klabu mbali mbali kutoka mikoa ya Tanzania Bara,Zanzibar na klabu moja kutoka Nairobi nchini Kenya.

Kwa upande wake Ofisa Michezo wa Baraza la Michezo la Taifa Tanzania (BMT) NichoLaus Mihayo ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu wa Baraza hilo Neema Msitha, alisema amefurahishwa na ushindani ulioonyeshwa na waogeleaji hao.

"mashindano kama haya yatawapa nafasi waogeleaji kushiriki mashindano ya Taifa yatakayofanyika mwezi ujao, ninaomba wazazi na watanzania wakiunge mkono Chama cha kuogelea ili kukuza mchezo huu hapa nchini," lisema Mihayo.

# KAIRUKI ATAKA MATAMASHA MENGI KUCHOCHEA UTALII

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki ameshauri Mikoa na Wilaya zote nchini kuibua matamasha ya utalii na kutangaza fursa za uwekezaji katika maeneo yenye vivutio vya utalii lengo ikiwa ni kukuza utalii nchini.

Kairuki ametoa ushauri huo jana wakati akifunga rasmi tamasha la Utalii Same lenye Kaulimbiu "Alianzisha mama, Sisi tunamalizia" lilofanyika Wilayani Same, Mkoani Kilimanjaro.

"Kipekee nimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha sekta ya utalii na ukarimu inaendelea kukua na kuongeza mchango wake katika pato la taifa," alisema Kaituki na kuongeza,

"Nitumie fursa hii kuomba Mikoa na Halmashauri nchini kuendelea kushirikiana na wadau wa utalii katika kubuni matukio ya utangazaji Utalii kwa kuweka matamasha," alisema Kairuki.

Aidha, alisema Rais Samia alipokuwa mgeni rasmi katika tamasha la utamaduni lililofanyika mkoa wa Kilimanjaro mwaka 2022 alielekeza wadau wote wa utalii kushirikiana ili kuyaendeleza matukio ya namna hiyo katika kutangaza utalii.

Amempongeza Rais Samia kutokana na mafanikio katika sekta ya utalii yaliyotokana na Programu aliyoizindua ya 'Tanzania The Royal Tour' ambapo kwa mwaka 2023 Tanzania ilitembelewa na watalii 1,808, 205 kutoka watalii 1,454,920 waliotembelea nchini mwaka uliotangulia.

Kairuki alisema kufanyika kwa tamasha hilo ni utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025, Ibara ya 67 ambayo imeelekeza kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni tano na mapato yatokanayo na utalii kufikia Dola za Marekani bilioni sita.

"Ili kufikia malengo hayo ni lazima kila mmoja ahakikishe anawajibika katika nafasi yake hususani katika kutangaza utalii na fursa za uwekezaji, kutoa huduma bora kwa watalii ili waweze kurudi nchini, kuboresha miundombinu lakini pia kuendeleza uhifadhi." alisema Kairuki.



Kiungo wa Simba, Fabrice Ngoma (kushoto) akiwania mpira wa juu na Nahodha wa Asec Mimosas wakati wa mchezo wao wa kundi B hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika juzi usiku. Timu hizo hazikufungana. **PICHA: BINZUBERY**

## *Yanga yatinga robo fainali CAF kibabe*

INATOKA UK. 24

andika bao la pili kupitia kwa Aziz Ki kwa mguu wake wa kushoto baada ya makosa ya walinzi wa CR Beloizdad kabla ya kuporwa mpira.

Musonda alipachika la tatu dakika ya 49 ikiwa ni dakika mbili baada ya bao la pili kufuatia kazi nzuri ya Pacome aliyekimbia na mpira umbali mrefu kabla ya 'kuwachambua kama karanga' mabeki wa Belouizdad na golikipa wao na kutoa pasi kwa Musonda aliyeukwamisha wavuni kirahisi.

Guede aliyeingia robo ya mwisho ya kipindi cha pili, alipigigilia msumari wa mwisho kwenye jeneza la CR Beloizdad dakika sita kabla mechi kumalizika likiwa ni bao muhimu ambalo rasmi limeipeleka Yanga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa mashindano hayo.

# Simba mahesabu yote kwa Jwaneng Galaxy

INATOKA UK. 24

"Leo (jana) tumeanza maandalizi kuelekea mchezo wetu wa mwisho ambao kwetu ni kama fainali, kuna mambo mawili katika mechi dhidi ya Jwaneng Galaxy kutafuta ushindi utakaotupeleka hatua ya robo fainali na kulipa kisasi.

"Hii haitakuwa mechi ya kawaida bali ni fainali kwetu kuhakikisha tunafikia malengo yetu ya kwenda robo fainali kwa kumfunga mpinzani wetu huyo," alisema Matola.

Alisema kuwa hawataki kurudia makosa ya msimu wa 2020/2021 kwa kupoteza nyumbani dhidi ya Jwaneng Galaxy na ndio maana maandalizi ya mchezo huo yameanza mara baada ya kumalizika kwa mchezo dhidi ya Asec Mimosas.

"Tunarejea nyumbani tukiwa na kitu kimoja tu kichwani, mchezo dhidi ya Jwaneng Galaxy, tunaendelea kuwasoma wapinzani wetu kupitia michezo yao ya hivi karibuni waliyoicheza, dhamira yetu ni kuingia tena robo fainali na baadae nusu fainali," alisema Matola.

Akizungumzia mchezo wao wa juzi, Matola alisema walicheza vizuri sana kipindi cha pili na kama wangekuwa makini kwenye safu yao ya ushambuliaji basi wangepata ushindi kwenye mchezo huo.

"Kipindi cha pili tulirudi kwa kasi kwa kuliandama lango la Asec Mimosas, dakika ya 46 Sadio Kanoute alipoteza nafasi ya wazi baada ya kumzidi ujanja mlinda mlango lakini shuti lake lilitoka pembeni kidogo, lakini pia kuna nafasi Chama aliipata nayo tungeweza kunufaika nayo," alisema Matola.

Naye kiungo wa Simba, Clatous Chama alisema mechi haikuwa rahisi kwa sababu wapinzani walikuwa nyumbani na walihitaji kupata matokeo uwanja wa nyumbani.

"Ni pointi moja muhimu tumeipata, sasa tunarejea nyumbani kumaliza kile tulichokianza na kuhakikisha tunasonga mbele," alisema Chama.

Alisema wanarejea nyumbani kupambana kupata ushindi katika mchezo wa mwisho dhidi ya Jwaneng Galaxy.

Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again'aliwapongeza wachezaji kwa kupambana na kupata pointi moja muhimu dhidi ya Asec Mimosas .

"Mechi ya mwisho ya nyumbani Tanzania itakuwa zaidi ya fainali , kila shabiki ajiandae kwa mchezo huu muhimu," alisema Try Again.

Michezo
Jumapili Februari 25, 2024
Nipashe



## Wenger aionya Liverpool kuhusu kocha

UKU. 22



Kiungo wa Yanga, Pacome Zouzoua (katikati) akiwatoka mabeki wa CR Belouizdad kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi kwenye uwanja wa Benjamini Mkapa, Yanga ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

## Simba mahesabu yote kwa Jwaneng Galaxy

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kupata pointi moja kwenye mchezo wa kundi B wa marudiano Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas, Simba sasa inapigia mahesabu mchezo wao unaofuata dhidi ya Jwaneng Galaxy ambao utatoa ramani kamili kama wanasonga hatua ya robo fainali au safari yao inaishia hapo.

Juzi Simba ikiwa ugenini ilifanikiwa kuwabana wenyeji wao na kulazimisha kumaliza mchezo 0-0 na hivyo kuendelea kushika nafasi ya pili kwa kundi lao wakiwa na pointi sita wakizidiwa pointi tano na Asec.

Ili kusonga mbele na kuingia hatua ya robo fainali, Simba italazimika kupata ushindi wa lazima kwenye mchezo wao wa mwisho dhidi ya Jwaneng Galaxy utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Machi 2.

Mara ya mwisho kwa timu hizo kukutana nchini Tanzania kwenye uwanja huo ilikuwa msimu wa 2020/21 ambapo Simba walikubali kipigo cha mabao 3-1 na kuondolewa hatua ya awali ya michuano hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Suleiman Matola alisema wamemalizana na Asec Mimosas na sasa akili na mahesabu yao wanayaelekeza kwenye mchezo wa Machi 2.

"Haukuwa mchezo mwepesi, vijana wamepambana na kufanikiwa kupata alama moja muhimu, tangu tunaingia uwanjani tulipanga kuwazuia wapinzani wetu wasipate bao, na hilo tumefanikiwa na kupata alama moja," alisema Matola na kuongeza,

INAENDELEA UK. 23

# Yanga yatinga robo fainali CAF kibabe

## ●●● Pacome Day yajibu, yaivuruga CR Belouizdad kwa Mkapa...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga jana ilifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kibabe baada kuwavuruga CR Belouizdad ya Algeria kwa kuwabebesha mzigo wa magoli 4-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ushindi huo wa kihistoria unaifanya Yanga kufikisha pointi nane ikishika nafasi ya pili kwenye Kundi D ikiiacha Belouizdad nafasi ya tatu ikiwa na pointi tano, Al Ahly inaongoza kundi hilo kwa kuwa na pointi tisa huku Medeama wakiburuza mkia wakiwa na pointi nne.

Kwa namna msimamo ulivyo na kanuni ya michuano hiyo inavyoeleza, Yanga hata akipoteza kwenye mchezo wao wa mwisho dhidi ya Al Ahly na Belouizdad akishinda mchezo wao wa mwisho dhidi ya Medeama watakuwa wamelingana pointi lakini Yanga ana faida ya kuwa na magoli mengi zaidi kati yake na Waalgeria hao itakapokuja maamuzi ya nani asonge mbele.

Kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa Algeria, Yanga ilikubali kipigo cha mabao 3-0 hivyo kama watalingana pointi kanuni inaweka wazi kuwa itaangaliwa kwanza walipokutana timu hizo mbili yaani 'head to head' nani alikuwa na matokeo mazuri zaidi.

Katika mchezo huo wa jana uliopewa jina la 'Pacome Day' na Kitengo cha habari cha klabu hiyo chini ya Afisa habari wake, Ali Kamwe, mabao ya Mudathir Yahaya, Stephane Aziz Ki, Kennedy Musonda na mshambuliaji mpya aliyesajiliwa kipindi cha uhamisho wa dirisha dogo, Joseph Guede, yalitosha kabisa kuimaliza Beloizdad ambayo ilikosa mbinu za kuupenya ukuta mgumu wa Yanga, uliokuwa ukiongozwa na Ibrahim Hamad 'Bacca' na Dickson Job.

Yanga iliuanza mchezo kwa kasi, wakipasiana pasi fupi fupi sehemu ya nyuma na katikati, lakini walikuwa wakiongeza kasi zaidi pindi wanapovuka mstari wa katikati kuelekea lango la wapinzani wao, hiyo ilionekana kama mbinu ya kutafuta bao la haraka.

Ilikuwa dakika ya nane ya mchezo, wakati Stephane Aziz Ki alipoupata mpira akiwa kiasi mita 30 kutoka lango la Belouizdad, aliachia shuti kali lililotoka nje kidogo ya lango.

Dakika mbili baadaye kilizuka kizaazaa kwenye lango la Belouizdad wakati Pacome Zouzoua alipowahadaa mabeki wa timu hiyo na kupiga krosi iliyombabatiza beki mmoja na mpira ukawa unaelekea wavuni, lakini ukaokolewa kwa ustadi mkubwa na golikipa, Alexis Guendouz ambaye aliupangua.

Mpira huo ukarudi kwa Yao Kouassi ambaye alipiga tena krosi iliyomgusa tena beki wa timu hiyo na kumpoteza uelekeo Kennedy Musonda ambaye alikuwa ameshajiandaa kuukwamisha wavuni.

Aziz Ki, kwa mara nyingine tena dakika ya 14 akiwa umbali na mita 28, aliupata mpira uliokuwa umekosewa na wachezaji wa CR Beloizdad, akatandika shuti kali ambalo lilimpita kipa, Guendouz, lakini mpira ukatoka nje.

Kipa huyo alifanya tena kazi ya ziada dakika ya 18, alipookoa michomo miwili mfululizo ya Pacome na Musonda.

Wakati kila mtu akiamini mechi itakwenda mapumziko timu zikiwa hazijafungana, Mudathir alibadilisha matokeo kwa kupachika bao dakika mbili kabla ya filimbi ya mwamuzi kwenda mapumziko.

Mpira ulioanza kwa Pacome, ambaye aliutuliza mpira na kuanza kukimbia kwa kasi kuelekea lango la wapinzani, akaupeleka mpira kwenye wingi ya kushoto kwa Lomalisa ambaye alikuwa amepanda kusaidia mashambulizi.

Beki huyo alipiga krosi ambayo haikuonekana kuwa na madhara sana kwani Musonda na wachezaji wengine wa Yanga walikuwa wanachungwa na mabeki wa CR Belouizdad, lakini Mudathir kwa kasi alitoka nyuma na kuuwahi mpira huo akaupiga kwa mguu wa kushoto, ukaenda kulia kwa kipa Guendouz, ambaye licha ya kuruka kutaka kuupangua, ukamshinda na kujaa kimiani.

Dakika mbili tu baada ya mapumziko, Yanga iliweka mpira ndani ya wavu, iki-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >